# SINTAKSIA YA KIJALIZO CHA KISWAHILI SANIFU: MTAZAMO WA X-BAA.

**LILY CHEBET KOECH**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**OKTOBA 2013**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa minajili ya shahada katika chuo chochote kile.

Sahihi…………………………………… Tarehe……………………………..

Lily Chebet Koech

## IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi tulioteuliwa na chuo.

Dkt. P. Jerono

SAHIHI……………………………………TAREHE…………………………………

Bw. B. G. Mungania

SAHIHI……………………………… TAREHE…………………………

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mume wangu mpendwa Anthony Kiruja Nyaga na watoto wangu wapendwa: Sandra Nyaga na Josephprince Nyaga.

Mapenzi, usaidizi na ushauri wenu ni chemichemi ya uvumilivu na bidii katika safari hii ya kiusomi.

## SHUKRANI

Kazi ya utafiti huwa si ya mtu mmoja; ni ya kikoa. Hivyo basi ningependa kutoa shukrani za dhati kwa watu mbalimbali waliofanikisha juhudi hizi. Kwanza, nawashukuru wasimamizi wangu, Dkt.Jerono Prisca na Bw. B. Mungania ambao waliufuatilia utafiti huu kwa makini hatua baada ya hatua na kunielekeza na kunikwamua nilikokuwa nimekwama. Uongozi na mawaidha ya busara waliyonipa yamenifungua macho katika maswala ya kiusomi kwa njia ya kipekee.

Pili, ninawashukuru wahadhiri wangu wote katika Idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu Cha Nairobi kwa kunifunza, kuniongoza, kunielekeza na kunihimiza katika safari hii ya kiusomi. Hawa ni pamoja na Dkt Andrew Mwenda Mbatiah, Dkt John Hamu Habwe, Dkt Kineene wa Mutiso, Dkt. Evans Mbuthia,Bw. B.Mungania, Dkt Iribe Mwangi, Dkt Zaja Omboga, Dkt Amiri Swaleh, Dkt George  Jefwa.

Aidha, natoa shukrani maalum kwa mjomba wangu, Bw. Daniel Koech na mkewe Roselyn Koech kwa kunilipia karo katika shule ya upili. Pia namshukuru mamangu mzazi kwa kunizaa na kunilea na kujitolea kwa hali na mali kunisomesha katika shule ya msingi. Aidha ninawashukuru kaka na dada zangu kwa kunihimiza kila mara nisome hadi ukomo wa elimu. Hao ni pamoja na: Evaline, Emily, Judy, Joan, Ben na Robin kwa kunihimiza kila mara nisome hadi ukomo wa elimu na kuamini kwamba nikifaidi tumefaidi sote.

Vilevile ninamshukuru Mwalimu mkuu wa Shule ya Wavulana ya Tengecha Bw John Koech kwa kuniruhusu kuendelea na masomo hasa kwa kuandaa ratiba ya kazi iliyoniruhusu kuhudhuria masomo bila kutatiza shughuli zangu kikazi.

Siwezi kamwe kuwasahau wanafunzi wenzangu, marafiki wangu wa dhati, Moraa Lydia, Keter na Merolyne Achiengambao daima tulihimizana na kuombeana katika safari hii. Wengine ni pamoja na Juliet, Jepngetich, Ndumbu, Chacha, Paul (mzee) Muriithi, Angeline,

Muniu, Rose, Maganga, Mary, Katutu, Suakei, George, Onyonka, Florence, Ken na Njeri. Undugu wetu darasani na nje ya darasa ulikuwa nguvu zisizo mfano.

Mwisho ninamshukuru Mungu kwa ulinzi na majaliwa yake kuniwezesha kusoma katika hali zilizokuwa ngumu, kuniongoza, kunihifadhi na zaidi kwa kunipa mada ya utafiti..

# MUHTASARI.

Utafiti wetu umechanganua kijalizo cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa. Tumepanua tafsiri ya kijalizo cha Kiswahili sanifu na kubainisha uamilifu wake katika tungo. Tumebainisha miundo tofauti ya vijalizo na kudhihirisha sheria zinazotawala uunganishwaji wa vipashio vinavyojaliza virai tofauti katika sentensi.

Sura ya kwanza inaweka wazi mada ya utafiti, sababu ya kuchagua somo, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, msingi wa kinadharia na yaliyoandikwa kuhusu mada.

Katika sura ya pili tumewekea msingi kazi yetu kwa kufafanua dhana tofauti ambazo tumetumia katika kuchanganua kijalizo. Dhana hizi ni kama vile, sintaksia, vishazi, virai na kategoria amilifu za sentensi.

Katika sura ya tatu tumechanganua miundo tofauti ya Kijalizo. Kijalizo kinaweza kuwa nomino au kirai nomino, kihusishi au kirai husishi, kivumishi au kirai vumishi, kitenzi au kirai tenzi. Pia tumejadili aina tofauti za kijalizo kwa msingi wa nadharia ya x-baa. Kwa mfano, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha nomino, kijalizo cha kivumishi kijalizo cha kihusishi na kile cha kielezi.

Katika sura ya nne, tumeandika matokeo ya utafiti, mapendekezo na mwisho , hitimisho.Tuligundua kuwa dhana ya kijalizo hueleweka kwa njia nyingi kutegemea mwelekeo wa nadharia inayotumiwa. Kijalizo katika sarufi mapokeo kilichukuliwa kuwa neno au fungu la maneno linalotokea baada ya kitenzi kishirikishi.

Katika utafiti wetu, tumetumia nadharia ya x-baa kufafanua kijalizo. Kijalizo katika nadharia ya x-baa ni neno au fungu la maneno linalofungamanishwa moja kwa moja na kichwa cha kirai husika (dada ya kichwa cha kirai). Kijalizo hupanua kichwa cha kirai hadi kiwango

kingine. Kwa mfano: Funga *huo mlango.* Maneno kwenye mlazo ni kijalizo cha kitenzi ‘funga’.

**VIFUPISHO**

N Nomino

T Kitenzi

W Kiwakilishi

V kivumishi

E Kielezi

H Kihusishi

KN Kirai nimino

KT Kirai tenzi

KV Kirai vumishi

KE Kirai elezi

KH Kirai husishi

Kij Kijalizo.

X Kategoria za maneno.

XP Kirai kamili cha X.

S Sentensi

$\bar{S}$ Kishazi kijalizi

**YALIYOMO.**

Ungamo……………………………………………………………...ii

Ikisiri……………………………………………………………..iii

Vifupisho…………………………………………………………iv

Yaliyomo…………………………………………………………..v

**SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi…………………………………………………………………1

1.1 Tatizo la utafiti…………………………………………………...3

1.2 Madhumuni ya utafiti……………………………………………….4

1.3 Nadharia tete………………………………………………………….4

1.4 Sababu za kuchagua mada……………………………………………4

1.5 Upeo na mipaka……………………………………………………….5

1.6 Msingi wa  kinadharia…………………………………………………6

1.6.1 Nadharia ya Eksibaa………………………………………………….7

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada…………………………………………18

1.7.1Yaliyoandikwa kuhusu nadharia……………………………………22

1.8 Njia za utafiti………………………………………………………….23

**SURA YA PILI**.

2.0 Sentensi na vipashio vyake………………………………………………………… 24

2.1 Utangulizi……………………………………………………….....................24

2.2 Dhana ya sintaksia……………………………………………………….......24

2.3 Vipashio vya sentensi…………………………………………………………25

2.3.1 Virai……………………………………………………………………………25

2.3.1.1 Kirai Nomino…………………………………………………………..27

2.3.1.2 Kirai Tenzi……………………………………………………………..30

2.3.1.3 Kirai Vumishi…………………………………………………………..32

2.3.1.4 Kirai Elezi……………………………………………………………….34

2.3.1.5 Kirai Husishi……………………………………………………………35

2.3.2 Vishazi……………………………………………………………….. .36

2.3.2.1 Vishazi huru…………………………………………………………….37

2.3.2.2 Vishazi tegemezi / vishazi vijalizi………………………………………....38

2.3.3 Kategoria amilifu za sentensi……………………………………………..40

2.3.3.1 Kiima……………………………………………………………………40

2.3.3.2 Kiarifa…………………………………………………………………..42

2.3.3.3 Yambwa / Shamirisho………………………………………………..43

2.3.3.4 Chagizo…………………………………………………………………45

2.3.3.5 Kijalizo…………………………………………………………………46

2.3.3.6 Hitimisho……………………………………………………………..47

SURA YA TATU.

3.0 Miundo na aina za vijalizo………………………………………………………..48

3.1 Utangulizi……………………………………………………………………48

3.2 Miundo ya vijalizo……………………………………………………………………..48

3.2.1 Nomino au Kirai Nomino…………………………………………………………….49

3.2.2 Kitenzi au Kirai Tenzi……………………………………………………………..51

3.2.3 Kihusishi au Kirai Husishi………………………………………………………….53

3.2.4 Kivumishi au Kirai Vumishi……………………………………………………….56

3.2.5 Kielezi au Kirai elezi……………………………………………………………….57

3.2.6 Kishazi kijalizi……………………………………………………………………..59

3.3 Aina za vijalizo……………………………………………………………………….60

3.3.1 Vijalizo vya Nomino……………………………………………………………….60

3.3.1.1 Kirai husishi kama kijalizo cha nomino……………………………………….62

3.3.1.2 Kishazi kijalizo cha Nomino…………………………………………………….65

3.3.2 Vijalizo vya vitenzi………………………………………………………………..66

3.3.2.1 Uteuzi wa Vitenzi……………………………………………………………….71

3.3.2.2 Vihusishi au Virai vihusishi kama kijalizo cha kitenzi…………………………78

3.3.2.3 Nomino pamoja na kihusishi kama kijalizo cha kitenzi………………………...81

3.3.2.4 Kitenzi kisoukomo kama kijalizo cha kitenzi…………………………………...82

3.3.2.5 Kitenzi kikuu kama kijalizo cha kitenzi kisaidizi……………………………….84

3.3.2.6 Vishazi vijalizi vya vitenzi………………………………………………......85

3.3.3 Vijalizo cha vihusishi……………………..........................................................88

3.3.3.1 Uteuzi wa vijalizo katika vihusishi…………………………………………...91

3.3.3.2 Kirai nomino, kirai elezi, kishazi kijalizi na kapa kama vijalizo vya vihusishi…92

3.3.3.3 Kihusishi kama kijalizo cha kihusishi kingine………………………………….96

3.3.4 Vijalizo vya vivumishi……………………………………………………………….97

3.3.5 Hitimisho……………………………………………………………………………..99

**SURA YA NNE**

4.0Matokeo ya utafiti…………………………………………………………………..101

4.1 Utangulizi……………………………………………………………………….101

4.2 Matokeo ya utafiti………………………………………………………………101

4.3 Mapendekezo…………………………………………………………………..102

4.4 Hitimisho………………………………………………………………………103

Marejeleo…………………………………………………………………………..104

## 1.0 UTANGULIZI.

Dhana ya kijalizo ni telezi. Maana yake imepanuliwa kadri nadharia za sintaksia zilivyoendelea kukua. Dhana hii ilianzishwa na wanasarufi mapokeo pamoja na dhana zingine walizoziita *Kategoria Amilifu za sentensi.* Maneno katika sentensi yaliainishwa kutegemea majukumu yaliyotekeleza. Wanasarufi mapokeo waligawa vipashio katika sentensi kulingana na majukumu kama:

a) Kiima

b) Kiarifu

c) Yambwa/ shamirisho

d) Chagizo

e) Kijalizo

Wanasarufi Mapokeo walieleza elementi kwa misingi ya maana na kusababisha utata (Habwe na Karanja 2004:143). Kiima kilielezwa kama sehemu ya kwanza ya sentensi ambayo huelezwa na kiarifu; kiarifu kikaelezwa kama sehemu ambayo huarifu kiima; yambwa kama nomino au kiwakilishi ambacho kinapokea kitendo katika sentensi; Chagizo kama neno au kikundi cha maneno kinachojaza nafasi ya kielezi katika tungo na kijalizo kama neno au kikundi cha maneno kinachofuata kitenzi kishirikishi. Maelezo haya yalikuwa na mushkili na yalikosa vigezo vya kisayansi (Habwe na Karanja 2004:143).

Crystal (1991), akinukuliwa na Obuchi na Mukhwana (2010:166), anasema kuwa dhana ya kijalizo hueleweka kwa njia nyingi kutegemea mwelekeo na nadharia inayotumiwa. Wanasarufi mapokeo walieleza maana ya kijalizo bila kuonyesha uamilifu wake kwa neno kuu katika virai tofauti. Katika nadharia ya x-baa, kijalizo kimepanuliwa kuwa sehemu ya kirai inayofafanua neno kuu katika kirai husika. Kirai nomino kimepanuliwa na kubeba kijalizo kinachokamilisha nomino; kirai tenzi kina kijalizo kinachokamilisha kitenzi; kirai

vumishi kimepanuliwa na kuwa na kijalizo kinachojaliza kivumishi na kirai husishi kupanuliwa kubeba kijalizo kinachojaliza kihusishi.

Kutokana na mielekeo tofauti inayotokana na nadharia tofauti, kuna mitazamo mbalimbali ya kufafanua kijalizo. Madai haya ya Crystal (ibid), yanadhihirika kwa tafsili tofauti zinazotolewa na wataalamu tofauti kuhusu kijalizo cha Kiswahili sanifu.

Habwe na Karanja (2004:164), wanasema kuwa kijalizo ni elementi nyingine katika kiarifu cha Kiswahili sanifu. Wanaeleza kijalizo kuwa ni neno ambalo hukamilisha kiarifu wakati ambapo kuna kitenzi kisicho na uarifishaji mkamilifu. Wanaendelea kwa kusema kuwa, ikiwa kijalizo hakitakuwepo, basi sentensi haitakuwa kamili.

Massamba (2004:33), anasema kuwa kijalizo ni kiambajengo muhimu cha sentensi au kishazi ambacho katika sarufi za kimapokeo kimechukuliwa kuwa na kazi ya kukamilisha maelezo yaelekezwayo na kitenzi. Anatoa mfano wa Kiingereza: *He broke the chair,* ambapo *the chair* ndicho kijalizo. Mfano katika Kiswahili: Mwajuma alipika *chakula.*

Matei (2008:124), anaeleza yafuatayo kuhusu kijalizo: kijalizo ni istilahi inayotokana na kitenzi 'jaliza' ambacho kina maana 'kamilisha'/ 'ongezea' habari ili kukamilisha au kutosheleza maana. Kijalizo ni neno/ kirai ambacho hufuata kitenzi kishirikishi na ambacho huelezea zaidi kiima au yambwa. Kijalizo huongezea maana/ hukamilisha maana ya kipashio kingine katika sentensi.

Nasi tunasema kuwa kijalizo ni kipashio kinachokamilisha kipashio kingine katika tungo. Ni kipashio muhimu katika tungo ili maana ya tungo iwe kamili. Hukamilisha nomino, kitenzi, kihusishi,kivumishi, kiima na yambwa. Kijalizo ni sehemu ya kirai inayofafanua kirai husika. Jackendoff (1977a:58) akinukuliwa na Radford (1988:236), anasema kuwa kijalizo ni kipashio chochote ambacho ni cha lazima katika tungo japo si katika miktadha yote.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Kumekuwako na tatizo la kufafanua kijalizo cha Kiswahili. Tunaamini utafiti wetu umesaidia kueleza na kufafanua dhana hii kwa mujibu wa nadharia ya x-baa. Kwa mujibu wa Obuchi na Mukhwana(2010), kuna mitazamo miwili tofauti ya kufafanua kijalizo ambayo ni:

(a) Maana pana inayojumuisha vipashio vyote vinavyotumika katika viarifa isipokuwa kitenzi.

(b) Maana finyu inayochukulia vijalizo kuwa maumbo yanayokamilisha sentensi zenye vitenzi vishirikishi.

Maelezo haya mawili yanayotofautiana yametupa motisha ya kutaka kufanyia utafiti wa kina kijalizo.

Mada yetu ya utafiti ni sintaksia ya kijalizo cha Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya X-baa. Tumechanganua kijalizo na kubaini miundo yake tofauti kwa kutumia nadharia ya X-baa. Kijalizo kinaweza kuchukua muundo wa kirai kama vile kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi,kirai elezi na kirai vumishi, au kategoria leksika kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, kihusishi. Aina za vijalizo ni nyingi. Kwa mfano, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha nomino na kijalizo cha kihusishi.

Utafiti wetu umeongozwa na maswali yafuatayo:

a) Je, ni  kweli kuwa kijalizo ni neno au kirai ambacho hufuata kitenzi kishirikishi? Ni kipashio cha kirai tenzi pekee?

b) Je, aina za vijalizo ni viwili pekee? Yaani kijalizo cha yambwa na kijalizo cha kiima?

c) Je, kijalizo kinaweza kuchanganuliwa kikamilifu kwa kutumia nadharia ya x-baa?

Katika utafiti huu tumechanganua muundo wa kijalizo ili kufanya uelewa wake kuwa wazi kabisa. Hii ni kwa sababu kufikia sasa utafiti unaohusu muundo wa kijalizo haujazingatiwa

kwa kina. Kwa hivyo utafiti wetu umenuia kuziba pengo na kupiga hatua ya kuainisha vijalizo kwa msingi wa uamilifu wake katika sentensi.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti huu tulinuia kufikia malengo yafuatayo:

(a) Kufafanua na kuipanua fasili ya kijalizo cha Kiswahili sanifu.

(b) Kuchunguza ili kugundua na kueleza sheria ambazo kwazo kijalizo kinajengeka.

(c) Kuchanganua vijalizo kikamilifu kwa kutumia nadharia ya x-baa.

## 1.3 NADHARIA TETE

Utafiti wetu umetathmini nadharia tete zifuatazo:

(a) Fasili finyu ya kijalizo cha Kiswahili sanifu haitoshelezi – kijalizo ni neno au kirai kinachofuata kitenzi kishirikishi.

(b) Kuna sheria ambazo zinatawala uunganishwaji wa vipashio vinavyojenga kijalizo.

(c) Kijalizo kinaweza kuchambuliwa kikamilifu kwa kutumia nadharia ya x-baa.

## 1.4 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO

Sababu zilizotupelekea kuchagua mada hii katika utafiti wetu ni kutokana na kuwa wataalamu wengi wana mitazamo tofauti kuhusu kijalizo. Wengine huchukulia kuwa kijalizo ni neno au fungu la maneno linalotumiwa kukamilisha kiarifu wakati ambapo kuna kitenzi kishirikishi. Wataalamu hawa wanadai kuwa kijalizo hakiwezi kutumiwa pamoja na kitenzi halisi Matei (2008). Tuliona kama maelezo haya ya kijalizo ni finyu na yalihitaji kupanuliwa zaidi. Jukumu la kijalizo ni kukamilisha kipashio kingine katika tungo. Tulitaka kuona iwapo maelezo haya yatafaa na iwapo yanafaa basi ni aina zipi za vijalizo zinazoweza kuainishwa?

Pili, kuchunguza ufaafu wa nadharia ya x-baa katika kuchanganua miundo ya vijalizo katika Kiswahili sanifu.

Tunaamini kazi hii imetoa mchango katika hazina ya tafiti zilizofanywa kuhusu lugha ya Kiswahili. Kazi yenyewe itawafaa wasomi na wataalamu wa Kiswahili kwa sababu itapanua uelewa wao wa dhana ya kijalizo.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Sentensi za Kiswahili huwa na sehemu tofauti za kiuamilifu kama vile kiima, kiarifu, yambwa au shamirisho, kijalizo na chagizo. Kijalizo ni mada yetu na tumechanganua mpangilio na uhusiano wake wa maneno kwa kutumia nadharia ya X-baa. Tumechambua miundo tofauti ya vijalizo katika sentensi kama vile muundo wa: kirai nomino, kirai tenzi, kirai vumishi na kirai husishi.

Tumepambanua pia aina tofauti za vijalizo kama vile: kijalizo cha kivumishi, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha nomino na kijalizo cha kihusishi kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Aidha tumetaja virai na kueleza kwa ufupi pasipo na kuingia ndani isipokuwa katika virai vile vinavyounda vijalizo vya Kiswahili. Vijalizo vya Kiswahili huchukua miundo tofauti ya virai kama vile virai nomino, virai husishi, virai tenzi, virai elezi na virai vumishi.

Utafiti wetu umejikita katika Kiswahili sanifu. Tumetumia nadharia ya X-baa kuchanganulia vijalizo ili kubaini mahusiano ya viambajengo vyake na pia mahusiano ya kijalizo na vipashio vingine katika sentensi ya Kiswahili sanifu.

Utafiti wetu umechambua sentensi sahili na sentensi changamani. Hatujajihusisha na lugha zungumzi bali tumejifunga kwa lugha andishi kwa sababu aghalabu huwa sahili na huweza kuchanganuliwa na pia kwa sababu tumechota data ya utafiti wetu kutoka lugha andishi.

## 1.6 MSINGI WA KINADHARIA

Lugha na matumizi yake ni maswala ambayo yamechunguzwa kwa muda mrefu na wanaisimu mbalimbali. Kuanzia miaka ya hamsini Chomsky amejaribu kupendekeza nadharia mbalimbali za sarufi. Mwaka wa 1957 alibuni nadharia ya sarufi miundo na mwaka wa 1963 akaifanyia marekebisho na kuibuka na nadharia ya sarufi zalishi geuza maumbo. Kufikia miaka ya sabini, mabadiliko yakafanywa na kukawa na nadharia ya wastani ambayo baadaye ilirekebishwa na kuwa nadharia ya wastani panuzi. Changamoto za kiuchanganuzi zilizojidhihirisha katika lugha kwa kutumia nadharia hizi zilimpelekea Chomsky kuibua nadharia ya Umilikifu na Masharti ambayo ndani yake kuna vinadharia vidogo vidogo. Vinadharia hivi ni:

a) X-baa- X-bar Theory.

b) Thita- Theta Theory.

c) Utawala – Bounding Theory.

d) Umilikifu - Government Theory.

e) Masharti- Binding Theory.

f) Uhusika- Case Theory.

Hata hivyo kuna wale wanaosema kuwa mwasisi wa nadharia ya eksibaa ni John Ross. Kuna wale wanaosema kuwa ni Jackendoff Ray (1977a) (Jerono 2003). Wanaisimu walioandika kuhusu nadharia ya Umilikifu na Masharti wamerejelea sana kazi ya Jackendoff (ibid), kwa mfano, Radford (1988), Cowper (1992), Haegeman (1991). Lakini kama tulivyokwisha kutangulia kusema, Chomsky alianza kuandika kuhusu nadharia ya Umilikifu na Masharti katika kazi yake ya 1970 aliyoiita, “Remarks on Nominalisation”. Kwa hivyo, kwetu sisi, mwasisi ni Chomsky (1970).

Nadharia tutakayotumia katika utafiti wetu ni ile ya eksibaa.

### 1.6.1 NADHARIA YA EKSIBAA (X-BAR THEORY)

Nadharia ya X-baa ilitangulizwa na Chomsky (1970) na inashughulikia jaribio la awali kabisa la kupata suluhisho la tatizo la sarufi miundo virai. Nadharia hii ya X-baa inatokana na upungufu ulioonekana kuwepo katika nadharia ya sarufi miundo virai. Nadharia hii ya sarufi miundo virai ilikuwa na kanuni nyingi zilizohusisha kategoria mbalimbali katika uwakilishi wa miundo ya sentensi.

Nadharia ya X-baa ni nadharia ya sarufi miundo iliyoendelezwa badala ya ile ya sarufi miundo virai. Hoja muhimu katika nadharia hii ni kwamba sheria za sarufi miundo virai hazina budi kuthibitiwa; na kwamba kategoria zaidi za virai hazina budi kuongezwa. Kwa mfano katika kategoria ya virai nomino kuna haja ya kuingiza kategoria nyingine ambazo ni kubwa kuliko nomino lakini ni ndogo kuliko kirai (Massamba 2004).

Kwa mujibu wa Cowper (1992:19), udhaifu wa kanuni miundo virai ni kuwa kanuni hazikuthibitiwa na kwamba kanuni zilichukua muundo huru kama ifuatayo:

A→ X,

Ambapo A ni kategoria moja na X ni kategoria nyingi zinazofuatana. Nadharia kama hii iliruhusu kanuni miundo virai ambazo hazikuwa sahihi. Kwa mfano:

KN→ S KT

KH→ KN KT KIB

Cowper (ibid) anaendelea kusema kuwa, kinachohitajika ni nadharia inayobainisha kanuni miundo virai zinazoweza kutokea katika lugha asilia. Kanuni zenyewe zibanwe kabisa ili chochote kinachoruhusiwa kiwe kinatokea kwa hakika katika lugha husika. Nadharia inayohitajika ni ile inayobainisha kwa wazi miundo virai inayowezekana katika lugha.

Nadharia ya eksibaa hutumia alama saidizi ya x□, ya tarakimu ($x^1$) na $x'$. Radford (1988) alitumia alama saidizi ya $x'$ naChomsky alitumia alama saidizi ya x□. Njia hizi tatu ni tofauti lakini zinaeleza jambo moja. Waandishi wengine hutumia alama hizi kwa kubadilishana: kwa mfano, Jackendoff (1977a) anatumia alama saidizi ya $\bar{X}$ katika anwani (it is called $\bar{X}$ syntax) lakini katika kitabu kizima anatumia alama ya $x'$. (Radford 1988)

Radford (1988 :167), anasema kuwa kuna viwango vitatu vya kuchanganulia virai.

(i) Kategoria ya kiwango cha neno.

N= Nomino; T= Kitenzi; V= Kivumishi; H= Kihusishi; E= Kielezi

(ii) Kategoria ya kiwango cha kati. Kwa mfano:

$\bar{N}$= Nomino baa moja.

$\bar{T}$= Kitenzi baa moja.

$\bar{V}$= Kivumishi baa moja.

$\bar{H}$= Kihusishi baa moja.

$\bar{E}$= Kielezi baa moja.

(iii) Kategoria ya kiwango cha kirai. Kwa mfano:

KN= Kirai nomino.

KT= Kirai tenzi.

KV= Kirai vumishi.

KH= Kirai husishi.

KE= Kirai elezi.

Radford (1988), anabaini kuwa kategoria za kati huwa kubwa kuliko kategoria kileksia lakini ndogo kuliko kategoria kamili (Kirai kikuu). Kuna viambajengo vilivyo vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko Kirai nomino na jinsi ambavyo kuna virai vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko Kirai nomino, ndivyo kulivyo na:

(i) Virai vivumishi vilivyo vikubwa kuliko vivumishi lakini vidogo kuliko virai vumishi vikuu.

(ii) Virai elezi vilivyo vikubwa kuliko vielezi lakini vidogo kuliko virai elezi kamili

(iii) Virai husishi vilivyo vikubwa kuliko vihusishi lakini vidogo kuliko virai husishi kamili.

(iv) Virai tenzi vilivyo vikubwa kuliko vitenzi lakini vidogo kuliko virai tenzi kamili. TY. Radford (1988 :227).

**Mifano katika sentensi**

1(a) John ni [ KN yule mwanafunzi wa Hisabati].

(b) Yeye ni [KV yule mpenzi wa watoto wake].

(c) Aliwatuza [ $\bar{S}$ wale waliocheza vizuri].

(d)Mwizi alianguka [KH nje ya dirisha].

(e)Lazima [KT uwe umemwazia msichana yule].

Viambajengo vilivyofungiwa kwenye mabano ni vijalizo vilivyo na maumbo tofauti. Viambajengo hivi ni virai kamili na ndani yake pana virai vya kati kama ifuatavyo;

1 (a) Mwanafunzi = N (Kichwa)

Mwanafunzi wa Hisabati = $\bar{N}$(Kirai cha kati)

Yule mwanafunzi wa Hisabati = $\bar{\bar{N}}$(Kirai kamili)

(b) Mpenzi = V (Kichwa)

Mpenzi wa mtoto = $\bar{V}$ (Kirai cha kati)

Yule mpenzi wa mtoto = $\bar{\bar{V}}$ (Kirai kamili)

(c) Nje = H (Kichwa)

Nje ya dirisha = $\bar{H}$ (Kirai cha kati)

Nje ya dirisha = $\bar{\bar{H}}$(Kirai kamili)

(d) Unamwazia = T (Kichwa)

Unamwazia yule msichana = $\bar{T}$(Kirai cha kati)

Iwe unamwazia yule msichana = $\bar{\bar{T}}$(Kirai kamili)

Radford (ibid: 228).


Kutokana na mifano hapo juu, kila kategoria ya kirai kina kategoria leksika. Hii si sadfa; kirai nomino lazima kiwe na nomino, kirai tenzi lazima kiwe na kitenzi, kirai husishi lazima kiwe na kihusishi, kirai elezi lazima kiwe na kielezi na kirai vumishi lazima kiwe na kivumishi. Kipashio ambacho ni cha lazima katika kikundi fulani cha kirai, tunakiita 'kichwa' cha kategoria.Sifa za kichwa zinakuwa sifa za kirai chote. Kichwa huamua upatanisho wa kisarufi katika kirai. Kwa mfano:

Mama *m*zuri


Kiti *ki*zuri

Nomino *mama*na *kiti*zinaamua viambishi ngeli vinavyochukuliwa na vivumishi. Kwa kuzingatia KN, KT, KV, KE, na KH inawezekana kuwa na kirai ambacho kina kichwa pekee (Cowper 1992:21). Mfano katika mchoro 2 (a) na (b), 2(a) ina kirai nomino yenye nomino pekee na kirai tenzi yenye kitenzi pekee na 2(b) ina kirai tenzi yenye kitenzi na kivumishi.

2(a)





(b)




Katika virai vyote, yaani KN, KT, KV, KE, na KH, kipashio muhimu na cha lazima ni kichwa cha kirai. Vipashio vingine vyote ni huria (si vya lazima). Nadharia ya X-baa inaongozwa na dhana ya neno kuu (kichwa) katika kirai na uhusiano wake na vipengele vingine katika kuunda kirai. Katika nadharia ya X-baa, alama X hutumika kuwakilisha neno kuu katika kirai na (¯ ) au baa huwakilisha vipashio vifuatilizo vya neno kuu/ kichwa katika kirai husika. Na XP huwakilisha kirai cha X. $\bar{\bar{X}}$ na XP zinafanana na hutumiwa kwa kubadilisha kinadharia.

Tunaweza kujumlisha maelezo hayo yote hapo juu kwa kuchora kielelezo kifuatacho Radford (1988:229)


(3)




X ni kategoria ya maneno kama vile N (nomino), T (kitenzi), H (kihusishi), V (kivumishi) E (kielezi). Spesifaya na kijalizo si za kategoria leksia bali huwakilisha uamilifu na mahusiano; kwa hivyo ziko katika kitengo kimoja na kiima na yambwa. Spesifaya ni neno linalotumiwa pamoja na nomino (Habwe na Karanja 2004:4). Huitwa pia kibainishi wakati unarejelea kategoria yake (Radford 1988:229). Jukumu la kibainishi katika nadharia ya x-baa ni kupanua $\overline{N}$ hadi $\overline{\overline{N}}$ katika kielelezo tungo. Mabano yaliyowekwa kwenye spesifaya na kijalizo yanadhihirisha kuwa vipengee hivi ni huria (si vya lazima).

Nadharia ya X-baa inazingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi. Ni upangaji unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki kipi. Radford (1988), alitumia istilahi kama vile dada (viambajengo vilivyo katika ngazi moja), binti ya (inamilikiwa na), na shangazi (uhusiano usiotokana na kifundo kimoja). Istilahi hizi zinaweza kuelezewa vyema kwa kutumia mchoro ufuatao.


(4)



Katika mchoro wa (4) kibainishi ni dada ya $\bar{N}$ na dada hao wawili ni binti za $\bar{\bar{N}}$; (wanamilikiwa na $\bar{\bar{N}}$), chagizo ni dada na binti ya $\bar{N}$ na kijalizo ni dada ya N na binti za $\bar{N}$; chagizo ni shangazi ya N. Kijalizo hupanua N hadi $\bar{N}$; nacho chagizo hupanua $\bar{N}$ hadi $\bar{N}$; kibainishi hupanua $\bar{N}$ hadi $\bar{\bar{N}}$. Kutokana na maelezo haya, inadhihirika kuwa uchanganuzi wa X-baa unatusaidia kueleza uhusiano wa viambajengo kwa kuzingatia muundo pekee. Ufafanuzi zaidi unadhihirika katika kielelezo kifuatacho.

(5) Huyu mwizi wa tarakilishi kutoka Nairobi .

5




Kipashio KNkinamiliki vifundo vya kibainishi (kib) na $\bar{N}$ . Kifundo cha kibainishi na cha $\bar{N}$ ni cha kiwango kimoja (dada). N na KH (kijalizo) ni vipashio vya ngazi moja na vinamilikiwa na $\bar{N}$. $\bar{N}$ na KH (chagizo) pia ni vipashio vya ngazi moja na vinamilikiwa na $\bar{N}$.


Kwa kuzingatia maelezo ya mchoro (5), uhusiano baina ya nomino (N) na chagizo ni wa mbali. Lakini kuna uhusiano wa karibu sana kati ya kichwa (N) na kijalizo, hii ndiyo sababu haiwezekani kukitenganisha kijalizo na kichwa cha kirai na kukihamisha hadi mwisho wa kishazi. Kwa mfano:

(6) (a) Mwizi [wa tarakilishi] [kutoka Nairobi]

(b)*Mwizi [kutoka Nairobi] [wa tarakilishi].

Sentensi (6b) si sahihi kwa sababu kijalizo [wa tarakilishi] kimehamishwa mbali na nomino (kichwa) na kuwekwa mwishoni mwa kishazi. Ikiwakilishwa kwenye kielelezo cha matawi itakuwa:

(7)




Mchoro wa (7) si sahihi kwani unavunja kanuni isiyoruhusu mpitano wa matawi.Kanuni miundo virai haingedhihirisha kosa hili.

Hata hivyo, vipashio katika Kiswahili ni huru na ndio sababu unaweza kupata kijalizo ambacho kimesongeshwa mbali na kichwa cha kirai na sentensi ikasalia kuwa sahihi. Hali ikiwa hivi, kijalizo kinabadilika na kuwa chagizo kwa sababu hakitakuwa dada ya kichwa cha kirai kwenye kielelezo tungo. Kwa mfano:


(8)

(a) Babu ***wa Keiyo*** amefika.


(b) Babu mrefu mweusi ***wa Keiyo*** amefika.

‘Wa Keiyo’ katika (a) ni kijalizo cha nomino ‘babu’ lakini katika (b) si kijalizo kwa sababu imesongeshwa mbali na kichwa cha kirai. Ithibati kwenye kielelezo tungo (9) (a) na (b) hapa chini:

9 (a)





(b).




Katika mchoro 9(a) KH ni kijalizo kwa sababu ni dada ya N na kwa hivyo kinapanua N hadi $\overline{N}$ lakini KH katika 9(b) ni chagizo kwa sababu ni dada ya $\overline{N}$ kwenye kielelezo tungo na kinapanua $\overline{N}$ hadi $\overline{N}$ .

Uhusiano huu wa karibu kati ya kijalizo cha nomino na neno kuu unaweza kuonyeshwa kupitia kwa kielelezo cha matawi (8) ( Radford 1988:191).

(10)




D na E ni dada na wanamilikiwa na B (viambajengo vya B) lakini C ambayo ni chagizo ni shangazi ya D na kwa hivyo uhusiano wao ni wa mbali. Chagizo kinaweza kuhamishwa mbali na neno kuu bila ya kuathiri maana ya tungo.

Ifahamike kuwa, kijalizo cha nomino, kibainishi na chagizo cha kirai nomino ni viambajengo huria (si vya lazima). Vinaweza kuwepo au kuondolewa pasipo na kuathiri kirai nomino. Hata hivyo katika kirai tenzi, kijalizo ni kiambajengo muhimu lakini chagizo siyo. Tazama sentensi ifuatayo:

(11)

a) Jona alimfanyia [Mary vibaya] [jana asubuhi].

b) Jona alimfanyia.

Kirai *Mary vibaya* ni kijalizo na ni kipashio muhimu katika kukamilisha kitenzi *fanyia.* Lakini sentensi bado itakuwa kamilifu kimaana bila ya chagizo *jana usiku.*Maana sentensi 11(b) inaning'inia kwa sababu msemaji anaachwa katika maswali kama vile, Jona alimfanyia nani nini?

Jackendoff (1977:34), akinukuliwa na Radford (1988:259), alitoa kanuni ya miundo virai ambayo ni:

(12)

$$X^n \Longrightarrow \ldots X^{n-1} \ldots$$

Neno kuu katika kirai chochote linajulikana kama $X^0$ na kategoria kirai inayobeba $X^0$ inajulikana kama $\bar{X}$ au X-baa moja na kategoria inayobeba $\bar{X}$ ni $\bar{\bar{X}}$ au X-baa mbili. X ni kategoria za maneno kama vile:N, V, T, E, na H. $X^{n-1}$ inawakilisha $X^o$, $\bar{X}$au $\bar{\bar{X}}$ na alama za dukuduku zinawakilisha viambajengo vinavyoweza kuongezwa. Hata hivyo kanuni (12) haikuruhusu hali kama ifuatayo: $\bar{N} \rightarrow \bar{N}$ ambayo aghalabu hujitokeza katika uhusiano baina ya chagizo na $\bar{N}$.Hapo mwanzo tulitaja kuwa chagizo hupanua $\bar{N}$hadi $\bar{N}$na kwamba chagizo ni kiambajengo huria (si cha lazima).

Kanuni ya Jackendoff (1977) ikapanuliwa kuwa:


(13)

$X^n \rightarrow \ldots X^m \ldots$   (m=n or n-1), Radford (ibid:261)

Kanuni ya (13) inairuhusu ‘m’ kuwa katika kiwango sawa na ‘n’ au ‘n-1’. Kwa mfano (14) unaoonyesha uchamko huu (Olali 1998):

Yule mtoto mrefu mweusi mgeni.


Uchamko wa aina hii unajitokeza katika sintaksia ya x-baa kama katika mfano (14)




Kijalizo huweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia X-baa. Kijalizo ni kipashio kinachofafanua neno kuu katika kirai husika. Kanuni ya kijalizo ni:

$X^1$ XP*. Radford (1988:267)

Alama ya kinyota inarejelea idadi yoyote ya vijalizo. Hii ni kwa sababu virai vingine kama virai tenzi huchukua vijalizo zaidi ya moja. Kwa mfano: Juma alimwandikia [*Maria][ barua ndefu]*. Itawakilishwa ifuatavyo katika kielelezo cha matawi. (15)




**1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.**

Kuna kazi nyingi ambazo zilitusaidia katika kutayarisha tasnifu hii. Baadhi ya kazi hizo zimeshughulikia uchanganuzi wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu, ama

kisintaksia au kisarufi. Kuna kazi za kisarufi ambazo zimetupa mwanga mkubwa katika kuelewa vyema kijalizo kwa jumla. Tumefaidi pia kutokana na kazi ambazo zimeshughulikia nadharia ya eksibaa kama vile:

Radford (1988), amefafanua virai tofauti akitumia nadharia ya X-baa katika lugha ya Kiingereza. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu utafiti wetu unahusu virai vinavyofafanua neno kuu katika kirai husika tukitumia nadharia ya X-baa. Anaeleza kijalizo kuwa ni sehemu ya kirai inayofafanua neno kuu katika kirai husika. Maelezo hayo ni muhimu kwetu kwa sababu ameweka wazi maana ya kijalizo japo kwa Kiingereza.

Cowper (1992), anaeleza kijalizo kama dada ya X katika kategoria zote kuu. Anasema kuwa ijapokuwa mpangilio wa vipashio katika kirai tenzi ni huru zaidi kuliko vipashio katika kirai nomino, hakuna kipashio kinachoruhusiwa kuingia kati ya kitenzi na kijalizo chake. Anaendelea kusema kuwa kanuni muundo virai haingeweza kubainisha uhusiano wa karibu kati ya kitenzi na kijalizo.

Ramsay na wengine (1995), wameeleza aina tatu za vijalizo ambavyo ni kijalizo cha kiima, kijalizo cha yambwa na kijalizo cha kitenzi. Kazi hii ni kati ya kazi ambazo zilitupa ari ya kutaka kukiangalia kijalizo cha kitenzi. Kulingana na wao, yambwa tendwa na yambwa tendewa ni vijalizo vya vitenzi. Kwa mfano katika sentensi ifuatayo. *Mwalimu anaandika barua.* Barua ni yambwa tendwa na pia ni kijalizo cha kitenzi anaandika.

Olali (1997) kama mtafiti, ametumia nadharia ya x-baa na mchango wake umetuonyesha uhusiano wa dada katika uchanganuzi wa virai. Ameonyesha namna ya kuchanganua XP iliyo na virai vingi ndani yake.

Massamba (2004), anafafanua kijalizo kuwa ni kiambajengo cha sentensi au kishazi ambacho katika sarufi za kimapokeo kimechukuliwa kuwa na kazi ya kukamilisha maelezo

yaelekezwayo na kitenzi. Maelezo haya ni mapana kwani kinyume na wengine, Massamba hajafunga maelezo ya kijalizo kwa vitenzi vishirikishi bali amefafanua kwa kurejelea vitenzi vyote. Hata hivyo amefunga maelezo ya kijalizo kwa vitenzi. Kwa mujibu wa utafiti wetu jambo hili si sahihi kwa sababu kijalizo ni kipashio kinachokamilisha kipashio kingine kiwe kitenzi, nomino, kivumishi, kihusishi.

Radford (2004), anaeleza kuwa kijalizo ni neno au kirai ambacho kimefungamanishwa na kichwa cha kirai (dada ya kichwa cha kirai) na hupanua kichwa hadi kiwango kingine. Anasema kuwa uchaguzi wa kijalizo hutegemea sifa za kichwa cha kirai.Anafafanua pia kuhusu kishazi kijalizi ambacho hujaliza kitenzi au nomino. Maelezo haya yote yatatufaa kwa sababu tutachanganua kijalizo kwa kutumia nadharia ya x-baa.

Aidha Habwe na Karanja (2004), wanafafanua kijalizo kuwa ni neno ambalo hukamilisha kiarifu wakati ambapo kuna kitenzi kisicho na uarifishaji mkamilifu. Maelezo yao ni banifu. Wamebana ufafanuzi wa kijalizo kwa aina fulani tu ya vitenzi ilhali vitenzi vyote vina uwezo wa kubeba kijalizo. Kwa mfano *Amina anapika <u>ugali.</u>*Ugali hapa ijapokuwa ni yambwa tendwa kwa sababu ndio unapikwa, bado ni kijalizo kwa sababu inakamilisha kile ambacho kinaelekezwa na kitenzi.

Mumbo na Ngamia (2005), wamefafanua vitenzi na aina zake kwa kina. Vitenzi ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu ndivyo vinavyokamilishwa. Mifano yao ya vitenzi vishirikishi ni mingi na ilifaa katika kufafanua kijalizo cha kiima. Vitenzi vishirikishi ni kama vile; kwisha, kuja, kutaka, kuweza, kupasa, kubidi na kadhalika.

Jerono (2003), ameeleza kijalizo kuwa ni aina ya neno ambayo hukamilisha maana hasa katika vitenzi vishirikishi. Maelezo yake yaelekea kuwa katika kikundi ambacho Obuchi na Mukhwana (2010) walikiita chenye mwelekeo finyu. Hatutachukua mwelekeo huu kwa sababu ni banifu mno. Hata hivyo kazi yake itatufaa sana kwa maelezo yake ya kina

kuhusiana na kategoria za maneno, virai, vishazi na kategoria amilifu za maneno ya Kiswahili kama vile kiima, kiarifu, yambwa, kijalizo na chagizo. Maelezo haya ni muhimu katika kuwekea kazi yetu msingi.

Jerono pia ametumia nadharia ya x-baa katika utafiti wake wa kishazi kiarifu. Kazi yake imetusaidia katika kuelewa matumizi ya nadharia ya x-baa katika uchanganuzi wa viungo vya sentensi.Anasema kuwa nadharia ya x-baa inatumika kuelezea miundo ya virai ya kila lugha na ni miongoni mwa nadharia zinazotumika kuunda nadharia ya sarufi bia.

Matei (2008), anaeleza kategoria za maneno, virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Vipengee hivi vyote ni muhimu katika kuwekea msingi kazi yetu. Hata hivyo amefafanua kijalizo kwa njia finyu ya kukihusisha tu na vitenzi vishirikishi.Amefafanua aina mbili tu za vijalizo ambavyo ni kijalizo cha kiima na kijalizo cha yambwa. Kuna aina nyingine ya vijalizo kama vile kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha kivumishi, kijalizo cha kihusishi na kijalizo cha nomino.

Mbesa (2008), katika kazi yake amechanganua kishazi nomino cha Kiswahili. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu amefafanua vishazi vijalizi vya nomino na kitenzi. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu tunachanganua vijalizo vya Kiswahili kwa ujumla.

Obuchi na Mukhwana (2010), wameeleza kijalizo kuwa ni neno linalokamilisha kitendo kinachotajwa na kitenzi. Maelezo haya ni ya wazi na yanafaa katika kufafanua kijalizo cha Kiswahili sanifu, ijapokuwa maelezo yake yamehusisha kitenzi pekee. Wameeleza pia viambajengo vya vijalizo kuwa vinaweza kuwa vielezi au virai elezi, vihusishi au virai husishi, nomino au kirai nomino. Maelezo haya yatatufaa. Hata hivyo hawakutaja vitenzi au virai tenzi na kishazi tegemezi.

Obuchi na Mukhwana pia wamesema kuwa kijalizo kinaweza kuelezwa kwa namna mbili tofauti. Namna ya kwanza ni ile finyu inayoeleza kijalizo kuwa ni neno linalokamilisha

vitenzi vishirikishi kama vile; kuwa, ndi, ni na kadhalika, kwa mfano Juma ni daktari. Daktari hapa ni kijalizo kwa sababu inakamilisha kiima ambacho ni Juma. Mtazamo huu ni finyu sana kwa sababu maana ya kijalizo imefungwa kwenye vitenzi vishirikishi pekee. Mtazamo wa pili ni ule mpana unaodai kuwa kijalizo hujumlisha vipashio vyote vinavyotumika katika kiarifa isipokuwa kitenzi. Maelezo haya hata hivyo yana kasoro kwa sababu ya kusema kuwa kitenzi hakiwezi kujaliza. Kitenzi hujaliza na aghalabu hujaliza kitenzi kingine. Vitenzi visoukomo vinajaliza vitenzi vingine. Hivi ni kusema kuwa kuna kijalizo cha kitenzi. Kwa mfano *Mugambi anapenda kusoma*. Kusoma ni kitenzi kinachokamilisha kitenzi anapenda. Ijapokuwa Obuchi na Mukhwana wanasema ni mtazamo mpana bado maelezo yake yamebana maana ya kijalizo. Kasoro nyingine katika maelezo haya ni kuwa kijalizo kimehusishwa na kiarifa pekee.

Nyaga (2011), amechanganua kishazi elezi cha Kiswahili sanifu akitumia nadharia ya x-baa. Kazi hii imetufaa kwa sababu imetupa msingi wa nadharia ya x-baa. Amesema kuwa nadharia ya x-baa huzingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti tofauti.

### 1.7.1 **YALIYOANDIKWA KUHUSU NADHARIA.**

Radford (1988) ameeleza kuhusu nadharia ya x-baa.Anasema kuwa Nadharia ya X-baa inazingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi. Ni upangaji unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki kipi.Alitumia istilahi kama vile dada (viambajengo vilivyo katika ngazi moja), binti ya (inamilikiwa na), na shangazi (uhusiano usiotokana na kifundo kimoja). Kijalizo ni dada ya neno kuu la kirai (X) kwenye kielelezo tungo. Kijalizo hupanua X hadi $\bar{X}$.

Cowper (1992), anasema kuwa nadharia ya x-baa ilitolewa ili kufidia upungufu wa nadharia ya kanuni muundo virai ambayo ilihitaji kuthibitiwa. Anaeleza kuwa nadharia ya kanuni

muundo virai haikutambua uhusiano wa karibu kati ya kichwa na kijalizo chake. Anafafanua kuhusu uteuzi, yaani uwezo wa kategoria leksika kuchagua kijalizo katika tungo.

Radford (2004), anaeleza kuhusu uwili wa nadharia ya x-baa. Anasema kuwa kifundo hugawika katika matawi mawili pekee hivi ni kusema kuwa KN hakiwezi kuzalisha matawi matatu. Maelezo yake ni muhimu kwetu kwa sababu tutatumia kielelezo cha matawi kuchanganua kijalizo.

Haegeman (1991), katika kuelezea nadharia ya x-baa, ameeleza kuhusu na uchanganuzi wa virai kwa kuzingatia kategoria na vile vile uchanganuzi wa vishazi. Anasema kuwa katika nadharia ya x-baa kila kirai humilikiwa na kichwa leksika.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI.

Utafiti huu tuliufanya kwa kudurusu vitabu, majarida na majuzuu mbalimbali maktabani kwa mujibu wa kukusanya data. Tulisoma vitabu vinavyohusu nadharia ya eksibaa tunayoitumia ili tuweze kuielewa zaidi na jinsi ya kuitumia katika utafiti huu.

Tulisoma pia kazi zilizoandikwa kuhusu kijalizo kwa ujumla ili tujue waziwazi maana ya kijalizo, muundo wake, aina zake na jukumu lake katika sentensi. Katika kusoma huku tutahakikisha kuwa tumechuja mawazo ya wasomi wengine ili tuyalinganishe na kuyalinganua na mawazo yetu.

Baada ya usomaji wa kina, kama wasomi wa Kiswahili tulipata data yetu kwa kutunga sentensi sahihi za Kiswahili na kutumia nadharia ya x-baa kuichanganua.Sentensi tulizotunga zilitathminiwa na wasomi wenzetu ili kuthibitisha usahihi wake.Tutatumia uchanganuzi wa X-baa kudhihirisha ufaafu wa nadharia ya x-baa katika uchanganuzi wa data yetu.

## 2.0 SENTENSI NA VIPASHIO VYAKE.

### 2.1 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza tumebainisha tatizo letu la utafiti na kuliwekea madhumuni, nadharia tete na mikakati ya kulitatua. Tumeeleza pia nadharia ya X-Baa ambayo tutatumia katika kuchanganua kijalizo cha Kiswahili sanifu. Hata hivyo, hatuwezi kuingilia swala hilo moja kwa moja pasipo na kuwekea msingi kazi yetu. Katika sura hii tunanuia kuweka maswala yanayohusiana na tatizo la utafiti wetu wazi. Maswala haya ni kama vile: Sintaksia, Sentensi, virai, vishazi na Kategoria amilifu za maneno.

### 2.2 DHANA YA SINTAKSIA.

Sintaksia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchanganuzi, mpangilio na na uhusiano wa vipashio katika sentensi. Taaluma hii inahakiki namna maneno yanavyopangwa ili kuunda tungo na sentensi zenye maana katika lugha. Hii ni kwa sababu sentensi si kitu kilichopangwa kiholela. Bali ni mpangilio wa kidaraja unaofuata utaratibu maalumu ambapo sauti huunganishwa ili kuunda maneno na maneno kuunda virai, virai kuunda vishazi na vishazi kuwa sentensi ( Radford 1988.)

Sintaksia ni ngazi mojawapo ya ngazi za isimu iliyo kati ya mofolojia na semantiki na huchunguza muundo wa sentensi ya lugha na viambajengo vyake kama vile mofu, maneno, virai na vishazi. Vipashio hivi vina uhusiano mkubwa na huungana katika kuunda kipashio kikubwa kinachoitwa sentensi kama tulivyokwisha taja hapo awali. Viambajengo hivi huunganishwa kwa kufuata kanuni fulani. Hudhihirisha uhusiano uliopo kati na baina ya viambajengo vya sentensi kando na kuonyesha namna maneno ya aina aina hufuatana katika kuunda sentensi inayokubalika.

Taaluma ya sintaksia huchunguza kategoria mbalimbali za maneno kulingana na utendakazi wake katika sentensi. Kategoria hizi ni nomino, viwakilishi, vitenzi, vihusishi, vielezi, viunganishi, vivumishi na vihisishi. Kategoria hizi za maneno ndizo hutumiwa katika sentensi.Dhana zingine zinazojitokeza ni zile za kuigawa sentensi kulingana na uamilifu wa sehemu hizo. Kwa mfano kuna kiima, kiarifa, yambwa, kijalizo, na chagizo. Hapa ndipo tunapopata mada yetu ya utafiti.

## 2.3 VIPASHIO VYA SENTENSI.

Sentensi ni tungo kubwa zaidi kimuundo kuliko kirai na kishazi na husheheni maana kamili. Huainishwa kwa kuzingatia muundo na uamilifu (dhamira). Kwa kuzingatia kipengee cha muundo tuna aina tatu kuu za sentensi ambazo ni: sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano. Kwa kuchukulia kipengee cha dhamira tuna: sentensi za ombi, sentensi za amri, sentensi za taarifa, sentensi agizi na sentensi hisishi. Sentensi huwa na makundi mawili makuu yanayobeba virai tofauti. Kikundi cha kwanza ni kikundi nomino na cha pili ni kikundi tenzi. Ndani ya makundi haya kuna virai tofauti kama vile kirai vumishi, kirai nomino, kirai elezi, kirai tenzi na kirai husishi.

### 2.3.1VIRAI.

Ni neno au fungu la maneno lililodokeza maana lakini maana hiyo si kamilifu. Haina muundo wa kiima – kiarifu kama ule wa sentensi. Kinabeba tu sehemu ya sentensi. Kamusi ya Longhorn (2011), inadai kuwa kirai ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima – kiarifa. Massamba (2004:35), anadai kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima – kiarifu (yaani hakihusishi mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa.)

Culicover (1976:11), anadai kuwa kirai ni mfuatano wowote wa maneno katika lugha yoyote na maneno yenyewe ni ya kategoria fulani. Kuna mfuatano wa maneno ulio mfupi kuliko sentensi lakini ni ndefu kuliko neno moja. Kwa hiyo kuna virai vilivyo virefu kuliko neno moja lakini fupi kuliko sentensi. (ibid:14). Anaendelea kudai kuwa, sentensi pia ni ya kategoria fulani ya kirai kinachoitwa sentensi. Kirai pia kinaweza kuwa neno moja (ibid:13). Kwa mfano:

***Laileti*** ni mrembo.

Laileti ni kirai nomino ijapokuwa kimeundwa kwa neno moja.

Radford (2004:14), anadai kuwa kila kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai chote. Kwa mfano:

***Mwanafunzi*** wa Hisabati.

***Mwanafunzi*** (umoja) ni kichwa cha kirai na ndicho kinachoamua sifa za kirai husika.

Kirai huainishwa kimuundo kulingana na neno kuu/ kichwa cha kirai husika. Kwa mfano:

> Kirai ambacho neno lake kuu ni nomino/ au kiwakilishi huitwa kirai nomino, kwa mfano: *Mtoto huyu*. Hapa neno kuu ni mtoto,ndipo kirai hicho kikaitwa kirai nomino.

Kirai kinaelezwa kuwa ni tungo ambayo haihusishi kitendo na yule anayetekeleza. Uainishaji wa virai kimuundo hutegemea neno kuu katika kirai hicho. Kwa kufuata mkabala huu tuna aina zifuatazo za virai: virai nomino, virai vivumishi/ virai vumishi, virai vielezi/ virai elezi, virai vitenzi/ virai tenzi, virai vihusishi/ virai husishi.

### 2.3.1.1 KIRAI NOMINO (KN).

Hii ni aina ya kirai ambacho hufanya kazi kama nomino. Neno kuu la kirai nomino ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Hujengwa na nomino, viwakilishi pekee au pamoja na maneno mengine yanayohusiana na nomino au viwakilishi hivyo. Kirai nomino huweza kuundwa na:

(i) Nomino (kiwakilishi) na kivumishi (N+V), kwa mfano:

Mwalimu mwingine.

(ii) Kivumishi na nomino (kiwakilishi) (V+N) ,kwa mfano:

Hawa wanawake.

(iii) Nomino ya kitenzi jina na kivumishi (N+V), kwa mfano:

Kuimba kwao.

(iv) Nomino (kiwakilishi) na nomino (kiwakilishi) (N+N), kwa mfano:

Mama na baba.

(v) Nomino (kiwakilishi) pamoja na kirai husishi, kwa mfano:


Mtoto wa mwalimu.

Kirai nomino huweza kuwa kiima au yambwa (kitendwa/ kitendewa) au kijalizo katika sentensi. Kwa mfano;

(a) *Mji huo* una *wezi wengi*.

Mji huo ni kiima.

Wezi wengi ni kijalizo




(b) *Sisi sote* tulijaribu *maswali hayo.*

Sisi sote ni kiima.

Maswali hayo ni yambwa tendwa kimapokeo lakini kijalizo katika nadharia ya X-baa. Kwa hivyo kirai nomino katika sentensi za Kiswahili huwa na majukumu mbalimbali kisintaksia. Majukumu haya ni:

**(i) Kiima.**

Kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hutuambia ni nani/ nini kinachozungumziwa katika sentensi. Kwa mfano:

**Mkuu wa shule** amenipa kazi nyingi.

**(ii) Yambwa tendwa.**

Yambwa tendwa (kipozi) ni nomino ambayo huathiriwa na tendo moja kwa moja. Ni kijalizo cha kitenzi. Kwa mfano:

Mama hupika **wali**.

**(iii) Yambwa tendewa (kitondo).**


Yambwa tendewa ni nomino inayotaja mtu ambaye anaathiriwa na kitendo kwa njia isiyo ya moja kwa moja (anayefaidika au kuhasirika kutokana na kitendo). Ni kijalizo cha kitenzi. Kwa mfano:

Jamila aliwanunulia **watoto** wake zawadi.

**(iv) Kijalizo cha kiima.**

Kijalizo cha kiima ni kijalizo ambacho urejeshi wake ni kwa kiima. Hasa katika sarufi mapokeo.

Kalulu alikuwa **daktari mzuri**. Uwakilishi wake katika tungo utakuwa




**(v) Kijalizo cha kivumishi**.

Ni kijalizo ambacho kinajaliza kivumishi hasa cha ‘a’ unganifu.

Uongo wa **wanasiasa nchini** umedhihirika.

‘Wanasiasa nchini’ ni kirai nomino kinachokamilisha kivumishi ‘wa’.

**(vi) Kijalizo cha kihusishi.**

Kirai nomino ni kijalizo kinachokamilisha kihusishi. Kwa mfano:

Paka amelala juu ya **kitanda changu**.


‘Kitanda changu’ ni kirai nomino kinachokamilisha kihusishi ‘juu ya’.

### 2.3.1.2 KIRAI KITENZI (KT).

Kirai tenzi ni neno au kundi la maneno ambalo hufanya kazi pamoja kama kitenzi. Neno lake kuu huwa ni kitenzi. Kirai tenzi huweza kuwa na:


(i) Kitenzi kisoelekezi pekee kama vile:

Amelala.




*(ii)* Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu:

**Amekuwa akicheza**.




Amekuwa=kitenzi kisaidizi.

Akicheza=kitenzi kikuu.

(iii) Kitenzi na kielezi:

**Alimchapa vibaya sana**.

Alimchapa=kitenzi halisi.

Vibaya sana=vielezi (kirai elezi)

(iv) Kitenzi na nomino:

**Alirusha jiwe**.

Alirusha=kitenzi halisi/ kitenzi elekezi.

Jiwe=nomino.

(v) Kitenzi na kirai nomino na kirai husishi.

**Alimpigamtoto wa watu**.

Alimpiga=kitenzi elekezi.

Mtoto wa watu=kirai nomino.

Wa watu=kirai husishi.

Wa=kihusishi 'a' unganifu.

Watu=nomino.

(vi) Kitenzi na nomino na kirai vumishi.

Tom **alikulamuwa mtamu.**

Alikula= kitenzi elekezi.

Muwa mtamu=kirai nomino.

Muwa=nomino.

Mtamu=kivumishi.

(vii) Kitenzi na nomino na kirai elezi.

Makero **amekula ugali leo asubuhi**.

Ameenda=kitenzi elekezi.

ugali=nomino.

Kirai elezi=leo asubuhi.

(viii) Kitenzi na kirai husishi:

**Alipanda juu ya mti**.

Alipanda=kitenzi elekezi.

Juu ya mti=kirai husishi.

Juu ya =kihusishi.

Mti=nomino.

(ix) Kitenzi na kishazi kijalizi.

Riziki **aliwacheka kwamba hawakuweza kusoma**.

Aliwacheka=kitenzi.

Kwamba hawakuweza kusoma=kishazi kijalizi.

(x) Kitenzi kishirikishi na kirai vumishi.

Sandra **nimwerevu ajabu**.

Ni=kitenzi kishirikishi.

Mwerevu ajabu=kirai vumishi.

Kivumishi=mwerevu.

Kielezi =ajabu.

**2.3.1.3 KIRAI VUMISHI (KV).**

Virai vivumishi ni aina ya virai ambavyo muundo wake hujengwa kwenye kivumishi. Ni kikundi cha maneno chenye kivumishi (V) kama neno kuu. Kirai vumishi hufafanua nomino au kiwakilishi chake, kwa hivyo hufanya kazi kama kivumishi kimoja kifanyavyo.

Kirai kivumishi hujikita (hupatikana ndani ya) kirai nomino japo wakati mwingine hupatikana ndani ya kirai tenzi hasa kinapotumika pamoja na kitenzi kishirikishi. Hata hivyo ni muhimu kusisitiza kwamba kirai vumishi huwa na muundo uliobainika. Tazama:

**Miundo tofauti ya kirai vumishi.**

**(a)** Kivumishi pekee.

Mtoto **mzuri** amezaliwa.

Mzuri=kivumishi cha sifa.

**(b)** Kivumishi na vivumishi vingine.

Baba **mrefu mnene  mweupe** ni wa Mwende.

Mrefu, mnene na mweupe=kivumishi cha sifa

**(c)** Kivumishi na kielezi.

Mchezaji **hodari sana** ametuzwa.

Hodari =kivumishi cha sifa.

Sana=kielezi.

**(d)** Kivumishi na nomino.

Tunda **la limau** ni kali mno.

La=kivumishi cha ‘a’ unganifu.

Limau=nomino.

(e) Kivumishi na kishazi.

Mwalimu **mwenye garikubwa** amesafiri leo.


Mwenye=kivumishi cha pekee.

Kutufundisha vizuri=kishazi.

### 2.3.1.4 KIRAI ELEZI (KE).

Kirai elezi ni kirai ambacho neno lake kuu ni kielezi. Hakiundwi kwa kuwako uhusiano wa lazima kati ya neno kuu, yaani kielezi, na neno jingine lililoandamana na kielezi hicho. Hutumiwa kufafanua vitenzi, vivumishi na vielezi vingine. Kirai elezi huweza kuwa vya mahali, vya namna au hali, vya idadi au kiwango na vya wakati. Aghalabu hushika nafasi baada ya vitenzi. Kwa mfano:

Mwakumba alifika **jana jioni**.




Kirai elezi huweza kuundwa kwa:

(i) Kielezi pekee.

Niliamka **asubuhi.**

(ii) Vielezi zaidi ya kimoja.

Mzee alipika **vizuri sana.**

(iii) Kishazi elezi.

Aliniambia **alikotoka**.

(iv) Kielezi na kirai husishi.

Paka alilala **chumbani kando ya jiko**.

Kirai elezi kinaweza kutumika pamoja na kirai husishi, kwa mfano: kabla ya mkutano, mbele ya mwalimu. Kwa mfano:

Mkutano ulikamilika **usiku wa manane**.

Usiku=kielezi.

Wa manane=kirai husishi.

**2.3.1.5 KIRAI HUSISHI (KH).**

Kirai husishi ni kundi la maneno ambalo neno lake kuu ni kihusishi. Kirai husishi hutokea kama KN, KT au KE. Huwa sehemu ya kundi tenzi ambapo hufanya kazi kama vielezi. Endapo virai husishi vitajiri kama viambajengo vya KN basi hutekeleza wajibu kama vivumishi (kwa mfano: chakula *cha* mfalme). Hivyo, kirai husishi hutumiwa katika kuifafanua nomino sawa na kifanyavyo kivumishi.

Kirai husishi huweza kutokea popote katika sentensi, kwa mfano:

(i) Mwanzoni mwa sentensi.

*Licha ya kuchelewa kwao*, tulifanya mkutano.

Kichwa cha kihusishi ni *licha ya*.

(ii) Mwishoni mwa sentensi.

Huu ni mchanganyiko *wa mboga na maharagwe.*

Kichwa cha kihusishi katika sentensi (ii) ni *ya.*

**Majukumu ya kisarufi ya virai vihusishi**

Kirai husishi hutekeleza majukumu yafuatayo ya kisarufi:

1. Hutumiwa kufafanua nomino (kama kivumishi), kwa mfano:

(a) Majani *ya mti huo* yamenawiri.

(b) Kule *kwa Moraa* ni pazuri.

2. Hutumiwa kufafanua vitenzi (kama vielezi.)

   Tazama mifano;

   (a) Huenda tukahitaji kuishi *nje ya kijiji* kwa muda.

   (b) Tulimsikiliza mwalimu *kwa makini*.

3. Hutumiwa kama kiwakilishi (W) kwa mfano:

   (a) *Kwa Mokami* kuna majani mengi.

   (b) *Za kujengea* nyumba zimeharibika.

Miundo ya kirai husishi.

(i) Kihusishi na kielezi. Kwa mfano:

Jiwe **la pembeni** limetumiwa.

La=kihusishi.

Kielezi=pembeni.

(ii) Kihusishi na nomino.

Chakula **cha mtoto** kimeliwa.

Cha=kihusishi.

Mtoto=nomino.

(iii) Kihusishi na kishazi kijalizi.

Nimemsubiri **tangu alipoanza safari**.

Tangu=kihusishi.

Alipoanza safari=kishazi kijalizi.

**2.3.2 VISHAZI**

Kishazi ni kundi la maneno ambalo lina kiima kimoja na kiarifu kimoja. Kiima ni sehemu ya sentensi iliyo na nomino/ kiwakilishi na pengine maneno mengine. Kiarifu ni sehemu ya

sentensi ambayo ina kitenzi na pengine maneno mengine. Huitwa kiarifu kwa sababu ndiyo sehemu inayosema kilichofanyika kwa nomino. Kishazi kinaweza kuwa na kitenzi ambacho maana yake inakamilika au kitenzi ambacho hakijitoshelezi (hakina maana kamili.) Kitenzi ambacho hakijitoshelezi kinategemea kitenzi cha kishazi kingine ili kiweze kutoa maana kamili katika sentensi. Kuna aina mbili kuu za vishazi.

(a) Vishazi huru.

(b) Vishazi tegemezi.

**2.3.2.1 VISHAZI HURU.**

Vishazi huru ni vishazi ambavyo vina vitenzi vinavyoeleza maana kamili. Havihitaji vishazi vingine ili kuleta maana. Ni vishazi ambavyo hata vikiondolewa katika muktadha wa sentensi ambamo vimejikita huweza kujitegemea kama sentensi. Huitwa pia vishazi vikuu hasa vikiandamana na vishazi visivyoweza kujitegemea kama sentensi (vitegemezi). Kwa mfano:


**Mtoto** anayeimba **atasafiri leo**.

Vishazi vilivyokolezwa rangi ni vishazi huru (*mtoto atasafiri leo)* kwa sababu vinaweza kujitegemea kama sentensi hata vikiondolewa katika muktadha wa sentensi zinazozibeba. Matei (2008:201), anadai kuwa vishazi huru vinapotokea pekee kama sentensi huitwa sentensi sahili.

Miundo ya kishazi huru:

(i) Kitenzi pekee. Kwa mfano:

Ameenda.




(ii) Kirai nomino na kirai tenzi.

Amanda wa kale ameenda kazini.

Amanda wa kale=kirai nomino.

Wa kale=kirai husishi.

Amanda =nomino.

Wa=kihusishi.

### 2.3.2.2 VISHAZI TEGEMEZI/ VISHAZI VIJALIZI.

Hiki ni kishazi ambacho hakikamiliki, yaani hakijitegemei. Msomaji anahisi kuwa pana taarifa fulani ambayo haipo na inahitajika ili pawepo na maana kamili. Vishazi vitegemezi vinapata maana yake kamili vinapohusishwa na vishazi vingine vinavyoandamana navyo katika sentensi. Hata kishazi kitegemezi kinapoondolewa katika muktadha wa kishazi huru, bado kishazi huru kinaleta maana kamili. Kwa mfano:

<u>Kiprono alisema kwamba</u> tumbili hula nyasi.

Hata tukiondoa “Kiprono alisema kwamba” kishazi “tumbili hula nyasi” kitasimama kama sentensi inayojitegemea.

**Uainishaji wa vishazi vitegemezi**

Zipo aina mbalimbali za vishazi kulingana na vipashio vinavyoviunda. Kwa mfano:

**(a) Vishazi tegemezi vumishi/ virejeshi**

Hivi ni vishazi vinavyofanya kazi ya vivumishi. Huundwa kwa kirejeshi ‘amba’ au ‘O’ rejeshi. Vishazi rejeshi huturejesha nyuma kwa jambo lililozungumziwa.Vinaporejelea nomino, hufanya kazi ya kivumishi. Vishazi hivi vimekitwa kwenye virai vya maneno kama vile kirai nomino au kirai tenzi. Kwa mfano, Kitabu *kilichoraruka jana* kimetengenezwa.

**(b) Vishazi vitegemezi vya masharti.**

Hivi ni vishazi vitegemezi vinavyodokeza masharti yapasayo kutimizwa kabla kitendo hakijafanywa. Huundwa kwa viambishi vya masharti kama vile ki, po ya masharti, nge na ngali. Huweza pia kuundwa kwa maneno/ viunganishi vya masharti kama vile kama, iwapo, ikiwa. Kwa mfano, *Ikiwa utaendelea na tabia hiyo,* utaanguka mtihani.

**(c) Vishazi vitegemezi vya sababu.**

Vishazi hivi hueleza sababu ya kufanyika kwa kitendo. Huundwa kwa viunganishi vya sababu kama vile kwani, kwa vile, kwa sababu.Kwa mfano, Aliumia *kwa sababu alicheza vibaya.*

**(d) Vishazi vitegemezi vya walakini/ kinyume.**

Vishazi hivi hueleza hitilafu, hali au kasoro iliyo katika kitendo. Huundwa kwa maneno kama vile ingawa, licha ya, japo, ijapokuwa. Tazama mfano ufuatao,Tutafuzu *ingawa kuna vikwazo vingi.*

**(e) Vishazi vitegemezi vya kusudi**

Vishazi hivi hueleza kusudi la kufanya jambo. Hubainishwa kwa maneno yanayoleta maana ya kusudi la kutenda jambo fulani. Kwa mfano: *Ili tufaulu katika mtihani wetu,* lazima tutajitahidi zaidi.

### 2.3.3 KATEGORIA AMILIFU ZA SENTENSI.

Uamilifu ni jukumu au kazi ambayo inatekelezwa na vipashio mbalimbali katika sentensi. Maneno katika sentensi huweza kutekeleza majukumu makuu yafuatayo: kiima, kiarifa, yambwa/ shamirisho, chagizo,kijalizo.Sentensi za Kiswahili huwa na sehemu mbili kuu ambazo ni kiima na kiarifa.

#### 2.3.3.1 KIIMA.

Ni kipashio katika sentensi kinachohusika na utendaji wa tendo. Kirubi na wengine (2007:79), wanadai kuwa, kiima hutaja kitu, mtu au jambo linalozungumziwa katika sentensi yote. Kwa kawaida kiima lazima kiwe na nomino au kiwakilishi chake.Wakati mwingine kiwakilishi hicho hujitokeza kama umbo kapa. Sentensi yoyote haikamiliki pasina kiima, (Obuchi na Mukhwana 2010:167). Kiima hudokeza kile kilichozungumziwa katika sentensi. Hudhihirika kama neno moja (Bahati), au fungu la maneno (Bahati aliyefukuzwa jana).

Kiima kwa kawaida ndiyo mada kuu/ kiini cha sentensi au kishazi. Kiima ni kiambajengo cha kikazi katika tungo na hutaja mada inayozungumziwa. Mada inayorejelewa inaweza kuhusu mtu, mnyama, mahali au jina lolote.

**Aina za kiima.**

Kulingana na Massamba (2004:32), kuna aina zifuatazo za kiima:

(a) **Kiima ambatani** Ni kiima ambacho kina nomino au viwakilishi viwili, kwa mfano:<u>Asha na Chuku</u> wanakwenda sokoni.

(b) **Kiima dhahiri.**

Kiima kinachojitokeza waziwazi katika kuhusika na utendaji wa tendo.

*Emma* amesafiri leo.

**(c) Kiima fiche**

Kiwakilishi cha kiima ambacho kinarejea kwenye kiima kisicho dhahiri, kwa mfano, mofu {Ø } katika neno 'atacheza'.

**(d) Kiima mantiki.**

Neno ambalo ingawa haliko katika nafasi ya mwanzo ya sentensi lakini ndilo 'liwakilishalo' mtendaji wa tendo lililotajwa katika kitenzi, kwa mfano, sentensi: Wanafunzi wamefundishwa na mwalimu. Neno *mwalimu* ni kiima mantiki

**(e) Kiima sarufi**

Neno ambalo hutokea mwanzoni kabisa mwa sentensi na likiwa ndilo kichwa cha sentensi hiyo, kwa mfano katika sentensi, wanafunzi wamefundishwa na mwalimu, neno wanafunzi ndicho kiima sarufi.

Kiima huweza kuundwa na viambajengo vya kategoria kama vile nomino, kiwakilishi au kikundi nomino. Kiima huweza kuwa:

(a) Nomino/ kiwakilishi. Kwa mfano:

(1) Kirwa ameshiba.

(b) Nomino zaidi ya moja

(2) Juma na Omani wamepita mtihani.

(c) Nomino na kishazi rejeshi. Kwa mfano

(3) Sheria zilizotolewa zinafaa.

(d) Kishazi kirejeshi. Kwa mfano:

(4) Anayetaka kuniona, anione sasa.

(e) Kitenzi jina na maneno mengine. Kwa mfano:

(5) Kuruka kwake kulimchosha.

(6) Kuimba kwao kunafurahisha.

(f) Yambwa ya sentensi hiyo. Kwa mfano.

(7) Kitabu hicho kiliandikwa na Musyimi.

(g) Nomino au kiwakilishi na vivumishi.

(8) Shamba zuri litalimwa.

#### 2.3.3.2 KIARIFA /KIARIFU.

Ni sehemu ya sentensi inayoarifu kiima. Habwe na Karanja (2004:162), wanadai kuwa kiarifu ni sehemu ya sentensi ambayo inatoa taarifa kuhusu kiima. Kitenzi ni neno linaloonyesha jambo linalofanywa na kiima. Kulingana na Matei (2008:215), kiarifa hutoa taarifa ifuatayo kuhusu kiima.

(a) Kiima ni nini? Kwa mfano:

Rajabu ni daktari.

(b) Kiima kina nini? Kwa mfano:

Mtoto ana kitabu.

(c) Kiima kinafanya nini, kwa mfano:

Mulei anasoma gazeti.

(d) Kiima kinahisi nini.

Kipchoge ana uchungu.

Maneno muhimu yanayojitokeza katika kiarifu ni pamoja na, yambwa kijalizo na chagizo. Kuna uwezekano wa kiarifa kusimama pekee pasina kiima.

**Muundo wa kiarifu**

Ifuataayo ni baadhi ya miundo ya kikundi tenzi.

(a) Kitenzi kikuu halisi: Juma anacheza.

(b) Kitenzi kishirikishi au kitenzi kisaidizi: Juma ni mchezaji, Lyongo alikuwa anaimba.

(c) Kitenzi na shamirisho/ yambwa: Juma anasoma kitabu.

(d) Kitenzi na chagizo: Lora alichapwa vibaya.

#### 2.3.3.3 YAMBWA /SHAMIRISHO.

Yambwa ni kitendwa au kitendewa cha kitendo fulani. Wamitila (2004:264), anadai kuwa yambwa hutumiwa kuelezea nomino ambayo au ambazo huchukua nafasi ya anayepokea kitendo fulani yaani mtendwa au hata mtendewa. Yambwa hujulikana pia kama shamirisho.

Yambwa ni kiambajengo katika sentensi ambacho hutaja mtendwa, tendo na mtendewa. Yambwa hujitokeza kama nafasi inayokaliwa na nomino, kundi nomino, au kiwakilishi.

Kuna aina tatu za yambwa: yambwa tendwa (shamirisho kipozi), yambwa tendewa (shamirisho kitondo), yambwa ala (shamirisho ala). Yambwa tendwa/ shamirisho kipozi ni yambwa ambayo tendo au lengo limeelekezwa kwake moja kwa moja. Arege na Matei (2006:111) wanasema kuwa yambwa tendwa huashiria nomino/ kitu ambacho kitendo/ lengo huelekezwa kwake moja kwa moja. Ni nomino ambayo huashiria kitendwa katika sentensi. Kwa mfano: Mama anapika wali. Neno lililopigiwa mstari ni nomino ambayo inapokea kitendo husika moja kwa moja. Hujibu swali ‘nini’ na ‘nani’.

Yambwa tendewa/ shamirisho kitondo hutumika kuelezea nomino, jina la kitu au mtu ambaye anafanyiwa jambo. Ikiwa mtu anafanya kitendo fulani kwa nia ya kumfaidi mtu mwingine; huyo mwingine atakuwa yambwa tendewa, yaani hapokei tendo lililopo moja kwa moja. Massamba (2004:117), anasema kuwa yambwa tendewa ni yambwa ambayo inaathirika na tendo au lengo ingawa lengo au tendo hilo halikuelekezwa kwake moja kwa moja. Kwa mfano: Mwalimu amemuandikia mzazi barua.

Yambwa tendwa – barua.

Yambwa tendewa – mzazi

Yambwa ala/ kitumizi huashiria kitu au kifaa kinachotumiwa kutendea jambo. Kitumizi huhusiana na yambwa kwani kinatumiwa kutekeleza tendo linaloelekezwa kwa yambwa. Wamitila (2004:280), anadai kuwa shamirisho ala/ yambwa ala ni shamirisho inayotaja chombo kilichotumiwa kutendea kitendo fulani. Kimsingi shamirisho ala hudokezwa kwa kuwepo na vihusishi. Ni kifaa ambacho ingawa hakipokei tendo, kinafanikisha tendo. Kinahusika katika utendaji wa tendo. Kwa mfano; Mfinyanzi ametengeneza nyungu (kipozi) kwa udongo (ala).

Kwa ujumla tunapata kwamba yambwa:

(1) Hujibu swali ‘nini?’ ‘nani?’. Kwa mfano:

Kirui anapika uji.

(2) Hujibu swali ‘kwa nini?’ ‘kwa niaba ya?’ kwa mfano

Baba amemjengea mama nyumba.

(3) Huweza kuwa nomino moja. Kwa mfano;

Oloo ameuza shamba.

(4) Huweza kuwa kirai nomino. Kwa mfano

Oloo ameuza shamba kubwa.

(5) Huweza kuwa nomino mbili. Kwa mfano

Bakari anawatumia Lila na Fila.

Huweza kuwa kiambishi. Kwa mfano:

Simbili amekukosea heshima.

(6) Huweza kuwa kiwakilishi. Kwa mfano:

Sitaki kukuambia yanayonisumbua.

(7) Kifaa kinachotumiwa kufanya tendo. Kwa mfano:

Alikata nyama kwa kisu.

### 2.3.3.4 CHAGIZO.

Chagizo ni sehemu ya sentensi inayoonyesha uhusiano wa uelezi –kueleza vipi, wapi, saa ngapi, na lini. Ni kipashio ambacho ni cha ziada (kisichokuwa cha lazima) na ambacho kinaweza kutolewa pasi na kuathiri maana iliyokusudiwa. Ipara na wengine (2010:106) wanasema kuwa chagizo ni neno au maneno katika sentensi yanayotoa taarifa kuhusu kiarifa (kitenzi) kwa kueleza au kutaja jinsi tendo lilivyotendeka, lini na wapi litakapofanyika. Chagizo mara nyingi huwa kielezi au kirai elezi au kirai husishi ambacho kinafanya kazi kama kielezi. Kwa mfano:

(a) Hao wamefika *kabla ya wengine* (chagizo ambayo ni kirai kihusishi).

(b) Weka jembe hilo *chini ya ghala* (chagizo ambayo ni kihusishi).

**Sifa za chagizo.**

Kwa kawaida ni kielezi au kirai husishi kinachofanya kazi ya kielezi na ni kipashio cha ziada.

Hutumiwa kufafanua kitenzi, kivumishi au kielezi. Kwa mfano:

(a) Chui hukimbia *haraka* (chagizo inayofafanua kitenzi).

(b) Mtoto huyu ni mrefu *sana*(ni chagizo inayofafanua kivumishi).

(c) Alicheza vizuri *mno* (chagizo inayofafanua kielezi).

#### 2.3.3.5 KIJALIZO.

Kijalizo ni kipashio kinachokamilisha/kinachojaliza kipashio kingine katika tungo. Massamba (2004:33), anaeleza kijalizo huwa ni kiambajengo muhimu cha sentensi au kishazi ambacho katika sarufi za kimapokeo kimechukuliwa kuwa na kazi ya kukamilisha maelezo yaelekezwayo na kitenzi kwa mfano: Jamila amepika ugali. Ugali ni kijalizo kwa sababu inakamilisha kitenzi 'pika'.

> Kijalizo ni istilahi inayotumiwa kurejelea uamilifu wa kisarufi jinsi ambavyo kiima kinadhihirisha uamilifu fulani wa kisarufi. Kijalizo ni neno au fungu la maneno lenye kuunganishwa moja kwa moja na kichwa cha kirai (dada ya kichwa cha kirai). Hupanua kichwa cha kirai hadi kiwango tofauti.TY . Radford (2004:329)

Kila kiarifu huwa na kitenzi. Hata hivyo baadhi ya viarifu huhitaji zaidi ya kitenzi kukamilisha sentensi. Baadhi ya maneno ambayo huhitajika kukamilisha sentensi yaliitwa yambwa kimapokeo lakini katika Umilikifu na Masharti yakaitwa kijalizo. Yambwa kwa hivyo pia hufanya kazi ya kijalizo. Yaani kukamilisha kitenzi. Kwa mfano:

Sara alimwandikia Yurabibarua.

Kuna aina tofauti za kijalizo kama vile kijalizo cha kiima, kijalizo cha kivumishi, kijalizo cha yambwa, kijalizo cha kihusishi, kijalizo cha nomino na kijalizo cha kitenzi.

Aina hizi za kijalizo zitafafanuliwa baadaye katika sura ya tatu.

### 2.3.3.5 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeweka wazi dhana ambazo tutatumia katika utafiti wetu. Tumefafanua dhana ya sintaksia, virai kama vile: kirai nomino, kirai tenzi, kirai vumishi, kirai elezi na kirai husishi. Tulipambanua pia miundo tofauti ya virai. Tulifafanua vishazi na aina zake tofauti kama vile vishazi huru na vishazi tegemezi.Tulieleza kategoria amilifu za maneno kama vile: kijalizo, yambwa, chagizo, kiarifa na kiima.

## 3.0 MIUNDO NA AINA ZA VIJALIZO.

### 3.1 UTANGULIZI.

Katika sura ya pili, tulijadili dhana tofauti ambazo tutatumia katika utafiti wetu. Tumefafanua dhana ya sintaksia kwamba ni mojawapo ya ngazi za isimu iliyo kati ya mofolojia na semantiki na huchunguza muundo wa sentensi ya lugha na viambajengo vyake kama vile mofu, maneno, virai na vishazi. Dhana zingine tulizojadili ni pamoja na: virai, vishazi na kategoria amilifu za maneno kama vile kiima, kiarifu, chagizo, na kijalizo. Katika sura hii, tutafafanua miundo tofauti ya kijalizo na aina zake tofauti kwa mujibu wa nadharia ya X-baa.

### 3.2 MIUNDO YA VIJALIZO.

Kijalizo ni kipashio kinachokamilisha kipashio kingine katika tungo. Mitazamo tofauti ya kijalizo yako katika 1.4. Kijalizo hutokea katika miundo tofauti. Kinaweza kutokea kama neno, kirai au kishazi. Kinaweza kuwa nomino au kirai nomino, kitenzi au kirai tenzi, kihusishi au kirai husishi, kivumishi au kirai vumishi, kielezi au kirai elezi.

Katika Kiswahili, vichwa vya virai hutangulia vijalizo vyake. Kwa sababu hii, Kiswahili ni lugha ya kichwa – kwanza. Radford (2004:15) Lugha kama vile Kikorea haitangulizi kichwa bali kijalizo hutangulia kisha kichwa lakini lugha ya Kiingereza inafanana na ya Kiswahili (kichwa kwanza kisha kijalizo baadaye). Kwa mfano:

Kiswahili: Funga ***huo mlango***.

Kiingereza: Close ***that door***.

Kikorea: ***Muneul*** dadara.

Door close.

Radford (2004:15)

Maneno yaliyokolezwa rangi ni vijalizo.

### 3.2.1 NOMINO AU KIRAI NOMINO.


Kijalizo kinachotokea kama nomino au kirai nomino kinatokea baada ya kitenzi ili kukamilisha kitenzi na baada ya kihusishi kusudi kukamilisha kihusishi. Kwa mfano:

(1) (a)Baba anasukuma ***rukwama mbovu***.

(b)Mtoto wa ***Rukia*** amepita mtihani.


***Rukwama mbovu*** katika 1(a) ni kijalizo kinachojaliza kitenzi na muundo wake ni kirai nomino. Katika (1) (b) ***Rukia*** ni nomino inayojaliza kihusishi ‘wa’. Mchoro 1(a) ni muundo wa kijalizo cha 1(a) katika kielelezo tungo na mchoro 1(b) ni nafasi ya kijalizo katika kielelezo tungo kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai kinachojalizwa.

1(a)





Mchoro 1(a) ni muundo wa kijalizo pekee. KV ni dada ya $\overline{N}$wala si dada ya N kwa sababu si kijalizo. Hakina jukumu la kupanua N hadi $\overline{N}$.

(b)




Mchoro 1(b) unadhihirisha muundo wa kijalizo kinapotokea pamoja na neno kuu la kirai ambalo ni kitenzi. Kirai nomino (KN) ni kijalizo cha kitenzi (T) na ndio sababu ni dada ya T katika kielelezo tungo. KN kinapanua T hadi $\bar{T}$ na ndilo jukumu la kijalizo. $\bar{T}$ kinajipanua hadi KT.

(1c)




Mchoro 1(c) ni muundo wa kijalizo kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai ambacho ni kihusishi (H). Kirai nomino (KN) ni kijalizo cha kihusishi (H). KN kinapanua H hadi$\overline{H}$ na $\overline{H}$ kinajipanua hadi KH.

### 3.2.2 KITENZI AU KIRAI TENZI.

Kitenzi au kirai tenzi pia hujaliza kitenzi kingine wakati ambapo kitenzi kisaidizi kimeandamana na kitenzi kikuu au kitenzi kisoukomo. Kwa mfano:


2(a) Halima alikuwa ***akicheza uwanjani***.

(b) Bahati anapenda ***kuomba.***

Kirai tenzi ***akicheza uwanjani*** na kitenzi kisoukomo ***kuomba*** ni vijalizo vya vitenzi husika.

Uwakilishi wake katika kielelezo tungo:


2 (a)(i)




Mchoro 2(a)(i) unaonyesha nafasi ya kijalizo kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai. KT(kirai tenzi) ni kijalizo cha Ts (kitenzi kisaidizi) kwa sababu KT ni dada ya Ts. KT (akicheza uwanjani) kinapanua Ts hadi $\bar{\bar{T}}$ na $\bar{\bar{T}}$ kinajipanua hadi KT.


Uwakilishi wa kirai kijalizi pekee (**akicheza uwanjani**) utakuwa:

2(a) (ii)




Katika mchoro 2(a) (ii), KE si dada ya T bali ni dada ya $\bar{T}$ . Hii ni kwa sababu KE si kijalizo bali ni chagizo kinachopanua $\bar{T}$ hadi $\bar{T}$.


2(b) (i)




Mchoro 2(b)(i) unaonyesha nafasi ya kijalizo kinapotokea pamoja na neno kuu la kirai ambalo ni Ts (kitenzi kisaidizi). Kijalizo ni KT(kirai tenzi) na ni dada ya Ts. KT kinapanua Ts hadi $\bar{T}$.

Uwakilishi wa kirai kijalizo pekee cha 2(b) utakuwa:

2(b) (ii)




Mchoro 2(b) (ii) ni muundo wa kijalizo pekee ambao ni kitenzi. Kitenzi (T) kinajipanua hadi $\bar{T}$na $\bar{T}$ kinajipanua hadi KT.

**3.2.3 KIHUSISHI AU KIRAI HUSISHI**.


Kihusishi hujaliza nomino na vitenzi katika tungo. Kwa mfano:

3(a) Titi ***la mama*** li tamu.

(b)Babu alikuwa ***kwa mtoto wake***.

***La mama***ni kirai husishi kinachojaliza nomino ilhali ***kwa mtoto wake*** ni kirai husishi kinachojaliza kitenzi. Uwakilishi wake kwenye kielezo tungo kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai ni:


3(a) (i)



Mchoro 3(a) (i) ni wa kijalizo (KH) kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai ambacho ni Nomino (N). KH ni kijalizo cha Nomino (N) na ndio sababu kinatokea kama dada ya N kwenye kielelezo tungo. Kijalizo (KH) kinapanua Nomino (N) hadi $\overline{N}$ na $\overline{N}$ kinajipanua hadi KN.

Uwakilishi wa kirai kijalizi pekee (**la mama**) utakuwa:


3(a) (ii).




Katika mchoro 3(a) (ii), ni muundo wa kijalizo cha nomino bila ya kichwa cha kirai ambacho ni Nomino (titi). KN (mama) ni kijalizo cha kihusishi (la) kwa sababu KN kimetokea kama dada ya H kwenye kielelezo tungo. KN kinapanua H hadi $\overline{H}$ na ndilo jukumu la kijalizo.

Sentensi 3(b) kwenye kielelezo tungo (muundo wa kijalizo kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai).


3(b)(i)




Mchoro 3 (b) (i) una kijalizo kilicho na muundo wa KH (kirai husishi). KH ni dada ya T (kitenzi) kwa hivyo ni kijalizo cha kitenzi. KH kinapanua T hadi $\overline{T}$ na $\overline{T}$ kinajipanua hadi KT.

Uwakilishi wa kirai kijalizi pekee (**kwa mtoto wake)**

3(b)(ii)




Kielelezo tungo 3 (b) (ii) ni muundo wa kijalizo cha kitenzi kinapotokea pekee kwenye kielelezo tungo. Muundo wa kijalizo chenyewe ni kirai husishi (KH). Ndani ya KH pana KN

ambacho ni kijalizo cha H (kihusishi). Hii ni kwa sababu KN ni dada ya H na kwa hivyo kinapanua H hadi $\overline{H}$ na $\overline{H}$ kinajipanua hadi KH.


### 3.2.4 KIVUMISHI AU KIRAI VUMISHI.

Kivumishi au kirai vumishi hujaliza kitenzi kishirikishi pekee. Vinginevyo,kivumishi huwa ni kipashio cha ziada (si cha lazima) katika tungo. Kwa mfano:

(4) Kondoo ni ***mjinga sana.***

Ni ***mjinga sana*** ni kirai vumishi kinachojaliza kitenzi ***ni***. Uwakilishi wake kwenye kielelezo tungo:


4(i)




Kielelezo tungo 4(i) kinaonyesha muundo wa kijalizo KV (kirai vumishi) kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai ambacho ni kitenzi (T). Kijalizo (KV) ni dada ya T (kitenzi) na kinapanua T hadi $\overline{T}$ na ndilo jukumu la kijalizo katika tungo.

Uwakilishi wa kirai kijalizi pekee kwenye kielelezo tungo(**mjinga sana** ):

**4(ii)**




Kijalizo KV (kirai vumishi) kina KE (kirai elezi) ndani yake lakini KE ni chagizo na wala si kijalizo kwa sababu ni dada ya $\bar{V}$.

**3.2.5 KIELEZI AU KIRAI ELEZI.**


Kielezi hufanya kazi ya kujaliza wakati ambapo kimetumika pamoja na kitenzi kishirikishi. Wakati mwingine pia hujaliza kihusishi. Kwa mfano:

(5) (a)Ali angali ***msikitini***.

(b)Habwe hutembea kwa ***haraka***.

***Msikitini*** ni kielezi kinachojaliza kitenzi na ***haraka*** ni kielezi kinachojaliza kihusishi ***kwa***. Uwakilishi wa 5(a) kwenye kielelezo tungo kijalizo kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai husika ni:


5(a)(i)




Katika mchoro 5(a) (i), kijalizo ni cha muundo wa KE. KE (kirai elezi) ni dada ya T (kitenzi) na kwa hivyo kinapanua T hadi $\bar{T}$ na ndilo jukumu la kijalizo.

Uwakilishi wa kirai elezi (kijalizo) pekee**:**


**5a(ii)**




Mchoro 5(a) (i) ni muundo wa kijalizo pekee ambacho kina muundo wa kirai elezi (KE).

Muundo wa kijalizo cha 5(b) kinapotokea pamoja na kichwa cha kirai kwenye kielelezo tungo utakuwa:

5(b).




Mchoro (b) una kijalizo chenye muundo wa kirai elezi (KE). KE ni dada ya H (kihusishi) na kwa hivyo kinapanua H hadi $\overline{H}$.


**3.2.6 KISHAZI KIJALIZI.**

Kishazi kijalizi hujaliza nomino na kitenzi. Kwa mfano:

Sijui **alipoenda Karimi**.

**Alipoenda Karimi** ni kijalizo cha kitenzi ‘sijui’.

Uwakilishi wake kwenye kielelezo tungo utakuwa:



### 3.3 AINA ZA VIJALIZO.

Kategoria kuu za maneno zina vijalizo vyake. Kuna:

(a) Kijalizo cha nomino.

(b) Kijalizo cha kitenzi.

(c) Kijalizo cha kihusishi.

(d) Kijalizo cha kivumishi.

#### 3.3.1 KIJALIZO CHA NOMINO.

Kijalizo cha nomino ni kijalizo ambacho ukamilishi wake hurejea kwenye nomino. Hukaribiana na nomino (neno kuu).Radford (1988:196), anasema kuwa kuna makundi matatu ya viambajengo vinavyovumisha nomino:

a) Kibainishi.

b) Chagizo.

c) Vijalizo.

i)Kibainishi hupanua $\overline{N}$ hadi $\overline{\overline{N}}$


ii) Chagizo hupanua $\overline{N}$ hadi $\overline{N}$ kwa kujirudia.

iii) Kijalizo hupanua N hadi $\overline{N}$.

Kikundi ambacho tutachambua ni cha kijalizo. Hata hivyo, katika Kiswahili si lazima kibainishi kipanue $\overline{N}$ hadi $\overline{\overline{N}}$ kwa sababu $\overline{N}$ inaweza kujiinua yenyewe hadi $\overline{\overline{N}}$. Kwa mfano:

*Mjane wa Simiyu* amesononeka.


‘Wa Simiyu’ ni kijalizo na kinapanua mjane hadi $\overline{N}$ ambayo ni ‘mjane wa Simiyu’. $\overline{N}$ nayo bila ya kibainishi inajipanua hadi $\overline{\overline{N}}$. Maelezo haya yanadhihirika zaidi kwenye kielelezo tungo hapa chini:




Aghalabu, nomino za Kiswahili hujalizwa kwa kirai husishi. Virai vinavyotokea baada ya nomino vinaweza kuwa kijalizo au chagizo kutegemea uamilifu wao. Tumekwisha eleza tofauti kati ya chagizo na kijalizo katika 1.6.1. Kwa mfano:

(6)Shirika ***la reli*** limefidiwa.

Katika sentensi (6) ‘shirika la reli’ ni kirai nomino na kichwa chake ni nomino ambayo ni ‘shirika’. Kijalizo cha nomino hapa ni kirai husishi ambacho ni ‘la reli’, kinajaliza nomino ‘shirika’. Pasipo na kijalizo, sentensi bado ni sahihi japo msomaji au msikilizaji anabaki kujiuliza maswali kama vile, shirika lipi?  Hasa kama msemaji hakuwa na ujumbe wa awali kuhusu kufidiwa kwa shirika lolote. Kirai nomino katika sentensi (6) kitawasilishwa ifuatavyo kwenye kielelezo tungo:




Katika mchoro wa sentensi (6), KH kinapanua N hadi $\overline{N}$ na $\overline{N}$ inajipanua hadi $\overline{\overline{N}}$. hivi ni kusema kuwa kirai KH ni kijalizo cha N.

**3.3.1.1 KIRAI HUSISHI KAMA KIJALIZO CHA NOMINO**.


Cowper (1992:25), anasema kuwa vihusishi vilivyo na uhusiano wa karibu sana na nomino ni vijalizo. Kwa sababu hii, Cowper anasema kuwa, kuna nomino ambazo zina sifa ya uelekezi kama za vitenzi elekezi. Kwa hivyo kuna nomino ambazo lazima zichukue kijalizo kihusishi ili maana ya tungo iwe kamili. Kwa mfano, unapotumia nomino 'mwanachama' lazima awe mwanachama wa kikundi fulani. Tazama sentensi (7).

7(a) *Mwanachama wa Bakita* amefutwa kazi.


(b) *Mwanachama* amefutwa kazi.

Sentensi 7(a) ni kamili kimaana, msikilizaji/msomaji haachwi na maswali kama katika sentensi 7(b) ambapo msikilizaji/msomaji anajiuliza maswali kama vile: mwanachama wa nini? Wa bunge? Wa sayansi? Wa mchezo? 'Mwanachama' lazima awe mwanachama wa kikundi fulani na usipotaja kikundi hicho, msikilizaji/msomaji atabaki akijiuliza maswali. Tofauti ya uwasilishi wa sentensi 7(a) na (b) katika kielelezo tungo 8(a) na (b) mtawalia ni:

8(a)





(b)




Katika mchoro wa 8(a), KH kinapanua N hadi $\bar{N}$, jukumu ambalo ni la kijalizo lakini N katika 8(b) haina kijalizo na kwa hivyo inajiinua hadi $\bar{N}$. Kielelezo tungo (9) kinaonyesha uchanganuzi wa kijalizo KH pekee.

(9)





Hata hivyo, kuna nomino ambazo hazina sifa za uelekezi. Kwa mfano:

(10) Mtu [mrefu] [mweusi] [mwenye upara kichwani] ameonekana akiiba

Virai vilivyo ndani ya mabano havijalizi N. Kwa hivyo katika kielelezo cha matawi, hakuna kirai ambacho kitakuwa dada ya N kwa sababu hakuna kijalizo. Nomino 'mtu' si elekezi na haihitaji kijalizo. Tazama kielelezo tungo (10):

(10)





### 3.3.1.2 KISHAZI KIJALIZI CHA NOMINO.


Nomino pia hujalizwa na kishazi kijalizi. Kwa mfano:

(a) Fununu ***kwamba uchaguzi utachelewa*** zilienea kote nchini.

(b) Uongo ***kuwa Diana ameiba kura*** haifai.

Maneno yaliyokolezwa rangi ni kishazi kijalizi cha nomino husika kwa sababu ni dada ya kichwa cha kirai kama inavyodhihirika katika vielelezo tungo vifuatavyo.




**3.3.2 KIJALIZO CHA KITENZI**.

Kijalizo cha kitenzi ni kijalizo ambacho ukamilishi wake hurejea kwenye kitenzi. Kitenzi kinaweza kuchukua kijalizo au kisichukue kijalizo kutegemea sifa zake za uelekezi. Kirai tenzi hujengwa kwa kitenzi pekee ingawa baadhi ya virai tenzi huhitaji zaidi ya kitenzi ili vikamilike. Maneno yanayotumiwa katika kukamilisha kitenzi katika kirai tenzi, kimapokeo yaliitwa *yambwa* lakini katika nadharia ya Umilikifu na Masharti yakaitwa *kijalizo.* Maneno

hayo hujiri kama nomino ama kiwakilishi chake na hupokea athari fulani katika sentensi. Maneno yanayotumiwa kujaliza kitenzi ni pamoja na:

(a) Nomino au kirai nomino.

(b) Kihusishi au kirai kihusishi.

(c) Kitenzi au kirai tenzi.

(d) Kishazi kijalizi.

Tutajadili nafasi ya vijalizo hivi katika kirai tenzi baadaye.

Vitenzi vya Kiswahili vinaainishwa katika makundi mawili kutegemea uwezo wao wa kuchukua vijalizo:

a) Vitenzi elekezi.

b) Vitenzi visoelekezi.

*Kitenzi kisoelekezi* ni kitenzi ambacho hakichukui kijalizo. Muundo wake haudokezi uwezekano wa kuwepo kwa kijalizo, kwa mfano:

(11)

a) Babu *alifariki*.

b) Mtoto *ametabasamu*.

c) Kikombe *kimeanguka.*

Vitenzi 'alifariki' 'ametabasamu' 'kimeanguka' ni vitenzi visoelekezi kwani havidokezi uwezekano wa kuwa na kijalizo. Vipashio ambavyo vinaweza kuongezewa ni vielezi na ambavyo si vya lazima. Kwa mfano:

(12)

a) Babu *alifariki jana*.

b) Mtoto *ametabasamu sana*.

c) Kikombe *kimeanguka vibaya.*

Maneno ‘jana’ ‘sana’ na ‘vibaya’ ni chagizo, yanafanya kazi ya kielezi katika tungo na si vipashio vya lazima na kwa hivyo hayawekewi vikwazo na vitenzi husika. Vitenzi katika (11)(a) na (b) haviwezi kuongezewa vijalizo maana ukifanya hivyo, utavuruga maana kama inavyoonekana katika (13) hapa chini:


(13)(a)*Babu *alifariki Maria*.

b) *Mtoto *alitabasamu wema*.


c) *Kikombe *kimeanguka mkono*.

Uwakilishi wa (11) (a) na (12) (a) katika kielelezo tungo na wa (14) (a) na (14)(b) mtawalia.

(14)a



(b)




Katika kielelezo cha matawi, kijalizo ni dada ya kitenzi na hupanua kitenzi hadi ($\bar{T}$). Katika kielelezo tungo (14) (a) T hakina kijalizo na kwa hivyo kinajiinua hadi $\bar{T}$. Katika (14) (b), T hakina dada na kama T katika (14)(a) kinajiinua hadi $\bar{\bar{T}}$. KE si kipashio cha lazima na ndio sababu hakitokei kama dada ya T badala yake kinapanua $\bar{T}$ hadi $\bar{T}$ kwa kujirudia. Michoro hii miwili inadhihirisha kuwa sentensi husika hazina kijalizo kwa sababu T hakina dada ya kuipanua hadi $\bar{\bar{T}}$.

*Kitenzi elekezi* ni kitenzi cha kutenda ambacho kinaweza kuchukua kijalizo. Muundo wake unadokeza kuwa kuna kinachoelekezewa tendo hilo. Kwa mfano:


(15)

a) Baba *alituandikia barua.*


b) Maria*alimposa Kibe*.

Unapotumia vitenzi elekezi bila ya kuongeza vijalizo (barua, Kibe) msomaji/msikilizaji anabaki na maswali kama vile: Baba aliandika nini? Maria alimposa nani? Kwa hivyo vijalizo ni vipashio vya lazima katika vitenzi elekezi. Uwakilishi wa sentensi 15(a) na (b) katika kielelezo tungo 16(a) na (b) mtawalia ni:

16 (a).




(b)




Katika vielelezo tungo 16(a) na (b), T kinapanuliwa na KN hadi $\bar{T}$ ikiwa na maana kuwa T ni dada ya KN. Ikiwa KN ni dada ya T basi ni kijalizo chake.


Kuna vitenzi elekezi ambavyo huchukua kijalizo chenye muundo wa KN zaidi ya moja kulingana na hali yake ya uambishaji. Kwa mfano:

(17) Baba alimjengea [mama] [nyumba nzuri]

Sentensi (17) ina kitenzi elekezi 'jengea' ambacho kinahitaji virai nomino viwili (vijalizo viwili) ili maana iwe kamili. Hii ni kwa sababu kitenzi 'jengea' kiko katika kauli ya kutendea. Lazima kuwepo na kijalizo kinachodhihirisha kitendwa na kitendewa. Katika

sentensi (17), kitendwa ni ‘nyumba nzuri’ na kitendewa ni ‘mama’. Sentensi (17) kwenye kielelezo tungo itakuwa:

(18)




Jackendoff (1977:58) akinukuliwa na Radford (1988:236), anasema kuwa vijalizo katika kirai tenzi ni vya lazima (ijapokuwa si kila wakati), lakini chagizo si cha lazima. Kwa hivyo, kipashio chochote ambacho ni cha lazima katika tungo ni kijalizo. Maelezo ya vitenzi na uwezo wake wa kuchukua vijalizo yanaelezwa kikamilifu kwa kuangazia **uteuzi wa vitenzi (verb subcategorization)**.

### 3.3.2.1 UTEUZI WA VITENZI.

Uteuzi hueleza aina za vijalizo ambazo neno huchagua. Kategoria zote kuu za maneno zina uwezo wa kuchukua vijalizo. Chomsky (1970) katika kazi yake ya mhadhara akinukuliwa na Radford (1988:146) anapendekeza kuwa kategoria kuu za maneno ni: Vitenzi, Nomino, Vihusishi, na vivumishi. Kategoria hizi kuu zinaweza kuelezwa kwa kuzingatia Nomino [± N] (ni Nomino au si Nomino), na Kitenzi [±T] (kitenzi au si kitenzi). Kwa kutumia

mapendekezo haya katika uteuzi wa vijalizo, kategoria kuu za maneno huwasilishwa ifuatavyo:

Kitenzi = [+T, -N]

Nomino = [-T, +N]

Kivumishi = [+T, +N]


Kihusishi = [-T, -N]

(Radford 1988:146).

Kategoria leksika hutueleza kuwa neno liko katika kategoria gani. Inaweza kuwa ni Nomino, Kitenzi, Kivumishi, au Kihusishi lakini kuna ujumbe mwingine kuhusu leksika ambao unatakikana kuhusishwa. Kamusi za zamani kama ya Hornby (1974), inahusisha si tu kategoria za maneno bali pia aina tofauti za vijalizo ambazo kategoria fulani za maneno huchukua (Radford 1988:339). Neno hupanga aina fulani za vijalizo ambazo linaweza kuteua. Ujumbe kuhusu aina za vijalizo ambazo neno linaweza kuchukuwa unaitwa *ujumbe wa uteuzi.*

Uteuzi wa vitenzi huamua ni kitenzi kipi kitatokea katika muktadha gani ( Cowper 1992:59). Zingatia mchoro ufuatao:

(19)




Katika kielelezo tungo (19) nafasi (?) inaweza kuchukuliwa tu na kitenzi elekezi kwa sababu mchoro una kijalizo ambacho ni ‘Mary’. Tazama sentensi (20) (a) na (b).

(20)(a) Juma anampenda/ anamdharau/ anamdhulumu/ anamuua Mary.

(b) *Juma anakufa/ anaanguka/ anatabasamu/ Mary.

Vitenzi katika (20) (a) vinateua kijalizo cha KN kwa sababu ni vitenzi elekezi kinyume na vitenzi katika (20)(b) ambavyo havina uwezo wa kuteua kijalizo (ni vitenzi visoelekezi).

Kielelezo kifuatacho kinaonyesha tofauti kati kitenzi elekezi na kitenzi kisoelekezi:

(21) (a) Anampenda: sifa za kategoria: [+T, -N];

Sifa za uteuzi: + [ _____ KN] (kitenzi elekezi)

(b) Kutabasamu: sifa za kategoria leksika: [+T, -N];


sifa za uteuzi: -[ _____ KN]. (kitenzi kisoelekezi)

Mstari wa kwanza katika (21) (a) na (21) (b) unatoa habari za kategoria ya neno, kwamba maneno ‘penda’ na ‘tabasamu’ ni vitenzi; mstari wa pili inatupa sifa za uteuzi za neno husika (uwezo wa neno kuchukua vijalizo). Kile ambacho sifa za uteuzi kinatuambia ni kuwa kitenzi ‘penda’ kinaweza kukalia nafasi [ ____ KN] na kwa hivyo kuwa na kielelezo: Sifa ya uchukuzi: [T, KN]; nacho kitenzi ‘tabasamu’ hakiwezi kukalia nafasi [_____ KN]

iliyoonyeshwa kwa kistari kirefu. Hii ni kwa sababu 'tabasamu' ni kitenzi kisoelekezi na hakiwezi kuchukua kijalizo.

Tumeeleza kuhusu vitenzi vinavyoteua vijalizo, lakini pia pana vitenzi ambavyo haviteui vijalizo. Tazama kielelezo tungo (22).

(22)




Sentensi ifuatayo itaeleza maana ya mchoro (22):

(23) Juma *ameanguka/ ametabasamu/ amekufa.*

Vitenzi katika (23) haviteui kijalizo, uteuzi wake ni kijalizo sifuri. Ni vitenzi ambavyo vinaweza kutumika bila ya kijalizo. Kielelezo cha maelezo haya ni:


24(a) Kufa: sifa za kategoria ni: [+T, -N];

sifa za uteuzi: [ ____ ] au [Ø]


24(a) inatueleza kuwa kitenzi 'kufa' kinaweza kutokea pamoja na kijalizo sifuri ikiwakilishwa kwa alama ya (Ø) ilhali 24(b) inatueleza kuwa kitenzi kufa kinaweza kutumika peke yake katika $\bar{T}$, bila ya kuandamana na kijalizo cha aina yoyote. Vielelezo vyote viwili vinadhihirisha kuwa kitenzi 'kufa' ni kitenzi kisoelekezi. Kwa upande mwingine kitenzi 'penda' katika (24) (a) hakiwezi kutokea pekee katika $\bar{T}$ na kwa hivyo hakiwezi kuonyeshwa

kuwa wenye uteuzi wa [ ___ Ø ] au [ ___ ] : hii inamaanisha kuwa hakiwezi kutumiwa bila ya kijalizo. Tazama vielelezo tungo (25) (a) na (b).

25(a)




25(b)




Katika (25) (a), kitenzi ‘penda’ lazima kipanuliwe na kijalizo hadi $\bar{T}$ lakini katika 25(b) kitenzi ‘tabasamu’ kinaweza kutokea katika $\bar{T}$ pekee bila ya kujalizwa.

Tumeona kuwa vitenzi ambavyo vinachukua kijalizo cha KN vinapewa sifa ya uteuzi ya [ ____KN], wakati ambapo vile ambavyo havichukui vijalizo vimepewa sifa ya uteuzi ya [ ___Ø] au [ ____ ]. Hata hivyo kuna vitenzi ambavyo ni elekezi na wakati uo huo si elekezi

(huchukua miundo ya uelekezi na usoelekezi). Kuna vitenzi kadhaa vya aina hii kama inavyodhihirika hapa chini.

26 (a) John hawezi kumpikia/ kumwelewa Maria.

(b) John hawezi kumpikia/ kumwelewa.

Vitenzi kama hivi vinapewa uteuzi wa vitenzi elekezi na visoelekezi. Njia moja ya kudhihirisha itakuwa kama ilivyo (27) hapa chini:

27) Pikia: Sifa za kategoria leksia: [+T, - N]

Sifa za uteuzi: [ ___ KN], [___Ø]


Kielelezo (27), kinadhihrisha kuwa kitenzi ‘pikia’ kinaweza kutumika pamoja na kijalizo cha KN na pia bila kijalizo. Njia nyingine ya kuwakilisha vitenzi vya aina hii ni:

Pikia: sifa za kategoria leksia: [+T,-N]


Sifa za uteuzi: [ __(KN)]

Mabano katika (KN) yanadhihirisha kuwa kitenzi, ‘pikia’ kinaweza kuchukua kijalizo au kisichukue (kijalizo si kipashio cha lazima katika kitenzi husika). Sentensi 26(a) na (b) zinaweza kuwasilishwa kwenye vielelezo tungo ifuatavyo:

28(a)




(b)




Katika mchoro 28(a), kitenzi ‘pikia’ kimejalizwa na kijalizo ‘Mary’. Kwa hivyo kijalizo kimepanua T hadi $\bar{T}$ lakini katika 28(b) T pekee inatumiwa katika $\bar{T}$.

Mpaka sasa tumeona kuwa kuna vitenzi vinavyochukua kijalizo cha KN kisha kuna vitenzi ambavyo vinaweza kuchukua kijalizo cha KN au kisichukue.

Tumechunguza vitenzi elekezi, visoelekezi na vitenzi vinavyobeba sifa zote mbili za uelekezi. Kuna ***vitenzi vingine ambavyo huchukua zaidi ya kijalizo kimoja***.


29) (a) Nilimpa [mwalimu wangu] [zawadi].

(b) Tarishi ali**ni**pa [barua].

Uteuzi unaofaa kwa vitenzi vya sampuli hii ni:

[ ___KN KN], kuonyesha kuwa vinaweza kuchukua vijalizo viwili vya KN. 29(a) na 29(b) katika kielelezo cha matawi:

**(30) (a)**




**3.3.2.2 VIHUSISHI AU VIRAI HUSISHI KAMA VIJALIZO VYA VITENZI .**

Ingawa tumeona tu uteuzi wa vitenzi kwa kurejelea vijalizo vya KN pekee, ni vyema kutaja kuwa, hata vihusishi ni vijalizo vya vitenzi japo si vihusishi vyote.Kuna vitenzi vinavyoruhusu kijalizo kihusishi kimoja au zaidi. Katika (31) hapa chini, vitenzi vinachukua vijalizo vihusishi tofauti vinavyoongozwa na vichwa tofauti vya vihusishi:

(31)

(a) Nimeenda [**kwa** nyanya].


(c) Mtoto ni [**wa** Mariamu].

(d) Tulitembea [**kando ya** kichochoro].

(e) Kibet alikuwa [**wa kwanza** mbioni].

Maneno yaliyo mabanoni ni virai husishi na ni vijalizo vya vitenzi. Vinajaliza vitenzi husika. Tazama kielelezo tungo kifuatacho:

(32)




Katika kielelzo tungo (32), KH ni dada ya T na kinapanua T hadi $\overline{T}$. Hii ni nafasi ya kijalizo.


Kutakuwa na tatizo la kubainisha vihusishi ambavyo ni vijalizo vya vitenzi. Hii ni kwa sababu mara nyingine vihusishi huweza kujitokeza kama chagizo au kama kijalizo. Kwa mfano:

(33) (a) Watalii wanapenda kutembea *kwaharaka sana*.

(b) Watalii wanapenda kutembea *kando ya mto*.


[kwa haraka sana] katika (33) (a) ni kirai husishi kinachofanya kazi ya chagizo wala si kijalizo (si kipengee muhimu katika tungo). Kinaweza kuondolewa katika tungo na maana ya sentensi isiathiriwe. Uhusiano wake na kichwa (T) si wa moja kwa moja kama inavyodhihirika katika kielelezo tungo (34):

(34)




Katika kielelezo tungo (34), KH si dada ya T badala yake ni dada ya $\bar{T}$ na KH hakipanui T bali kinapanua $\bar{T}$ hadi $\bar{T}$ kwa hivyo ni chagizo. Ni tofauti na kijalizo ambacho ni dada ya T na binti ya $\bar{T}$ kama inavyoonekana katika sentensi (33) (b) na katika mchoro (35) ufuatao:

(35)




[Kando ya mto] ni kirai husishi ambacho ni kijalizo na wala si chagizo. Katika mchoro (35), KH ni kijalizo kwa sababu ni dada ya T na kinapanua T hadi T-baa; hili ni jukumu la kijalizo. Kwa ujumla ni kuwa sentensi (33) (a) ina chagizo yenye muundo wa KH ilhali sentensi (33) (b) ina kijalizo chenye muundo wa KH pia.

Tofauti kuu kati ya kijalizo na chagizo ni kuwa kijalizo hutokea karibu na kichwa cha kirai husika kuliko chagizo. Tofauti nyingine ni kuwa kijalizo kinaweza kuwa cha lazima lakini chagizo daima si kipengee cha lazima katika sentensi. Vichwa vya virai huwekea vikwazo uteuzi wa vijalizo lakini hamna vikwazo vinavyowekewa chagizo kama tulivyokwisha kufafanua katika 1.6.1.

### 3.3.2.3 NOMINO PAMOJA NA KIHUSISHI KAMA VIJALIZO VYA KITENZI.

Mpaka sasa, tumebainisha vijalizo vya vitenzi vya aina mbili: vile vya KN na vile vya KH. Kuna vitenzi ambavyo vinachukua vijalizo vihusishi na vijalizo nomino pamoja katikasentensi moja. Mifano ifuatayo itadhihirisha kauli hii.

(36) (a) Johana alipeana [barua] [*kando ya/*tangu/ *miongoni mwa/ kwa mwalimu mkuu]

(b) Mwajuma alimlaumu [Kushi] [*katika/ *mkabala na / kwa kumsaliti]


Katika sentensi ya (36) neno la kwanza kwenye mabano ni kijalizo KN na neno la pili kwenye mabano ni kijalizo KH. Kutokana na mifano hii inabainika kuwa kitenzi kinachagua kihusishi kitakachochukua. Kwa mfano, kitenzi*peana* kinachukua kijalizo KH chenye 'kwa' lakini si kijalizo kihusishi chenye *kando ya, tangu, miongoni mwa*. Kitenzi kama *peana* kama kilivyotumika katika 36(a) kitakuwa na kielelezo kifuatacho.

(37) Peana: Sifa za kategoria: [+T,-N]

Sifa za uteuzi: [___KN [KH…kwa..]]

Ili kielelezo (37) kiwe sahihi tutaongeza ujumbe kuwa kihusishi 'kwa' lazima kiwe kimetumika kama kihusishi. Kielelezo (37) kinaonyesha kuwa kitenzi 'peana'kinaweza kuchukua kijalizo cha KH na na kijalizo cha KN na inapotokea, kijalizo KN kinatangulia kisha kijalizo KH hufuata kama inavyoonekana katika kielelezo tungo (38):

(38)




**3.3.2.4 KITENZI KISOUKOMO KAMA KIJALIZO CHA KITENZI**.

Kitenzi kisoukomo ni kitenzi ambacho hakina uambishi wa njeo, upatanishi wala idadi. Ni kitenzi ambacho aghalabu hutumika kujaliza kitenzi. Kitenzi kisoukomo hudhihirishwa kwa kuchukua kiambishi kisoukomo ‘ku’ na mara nyingine kiambishi cha yambwa. Mifano ya vitenzi visoukomo ni kama: kuruka, kucheza, kuuza, kusali, kuimba, na kulaghai. Vitenzi hivi huwa vijalizo vinapotumika sambamba na vitenzi vingine.


Radford (2004 :215), anadai kuwa vitenzi visoukomo ni vijalizo vinavyoonekana kama sentensi kamili. Naye Culicover (1976:11), anaeleza kuwa sentensi pia ni ya kategoria ya kirai. Kwa sababu hii tutachukulia kuwa kitenzi kisoukomo ni sentensi ambayo ni kirai tenzi kwa ajili ya uchanganuzi wetu. Kitenzi kisoukomo ni kijalizo kinachojaliza kitenzi kingine.

(39) (a) Ali anataka [kula maembe yote].

(b) Ali anataka [ku**ya**la maembe yote] *ya* ni kiambishi cha yambwa.

Uwakilishi wa sentensi (39) (a) katika kielelezo tungo utakuwa:

(40) (a)





[Kula] ni kijalizo cha kitenzi 'anataka'. KT kinapanua Ts hadi $\overline{T}$ (nafasi ya kijalizo).

Vitenzi visoukomo mara nyingine huitwa vitenzi vijalizi hasa kutokana na sifa yake ya kujaliza vitenzi katika sentensi za Kiswahili sanifu (Mbesa 2008). Radford (2004:40) anadai kuwa kitenzi kisoukomo kinatumika kujaliza vitenzi vingine kwenye tungo. Kwa mfano:

(41) Manyara anapenda [kuchezea wanawake]

Kitenzi *anapenda* katika (41) kinahitaji kijalizo ili kiwe kamili kimaana na kitenzi kisoukomo *kuchezea* kinakijaliza. Kitenzi kisoukomo hutumika kufafanua sehemu ya kishazi kikuu ambacho ni sentensi ya kimsingi. Kitenzi kisoukomo kinachojaliza kitenzi huchanganuliwa ifuatavyo katika kielelezo cha matawi:

(41)




Katika kielelezo tungo (41), kitenzi *anapenda* kinajalizwa na kitenzi kisoukomo *kuchezea* na ndio sababu ni dada ya T kwenye kielelezo tungo. Kwa hivyo kitenzi kisoukomo *kuchezea* nikitenzi.

### 3.3.2.5 KITENZI KIKUU KAMA KIJALIZO CHA KITENZI KISAIDIZI.


Kitenzi kikuu kinapoandamana na kitenzi kisaidizi, kinafanya kazi ya kujaliza kitenzi kisaidizi. Radford (2004:40) anadai kuwa vitenzi visaidizi ni vitenzi vinavyohitaji vijalizo ambavyo ni vitenzi ili maana yake iwe kamili. Kitenzi kijalizi chake ni kitenzi kikuu. Hutofautiana na vitenzi halisi ambavyo vinachukua aina tofauti za vijalizo. Kitenzi kisaidizi huruhusu kitenzi pekee kama kijalizo chake. Kwa mfano:

42 (a) Muturi alikuwa ***akilima.***


(b)Sungura angali ***anaiba mizabibu***.

Kitenzi ***akilima*** katika 42(a) na kirai tenzi ***anaiba mizabibu*** katika 42(b) ni vijalizo vya vitenzi husika. Kitenzi ***alikuwa*** na kitenzi ***angali*** vimetumika kama vitenzi visaidizi na vinajalizwa kwa vitenzi vikuu. Uwakilishi wake katika kielelezo tungo unakuwa:

43(a)




(b)




Katika kielelezo tungo 43(a) na (b), KT ni dada ya Ts na kwa hivyo, KT kinapanua Ts hadi kiwango cha $\overline{\overline{T}}$ na hili ni jukumu la kijalizo.

### 3.3.2.6 VISHAZI VIJALIZI VYA VITENZI.

Kuna vitenzi vinavyochukua vijalizo vinavyoonekana kama sentensi kamili, hutangulizwa na maneno kama vile: kwamba, kama, ua kuwa (Radford 2004:215). Vishazi vijalizi vya vitenzi vina sifa ya kutumika kama vijalizi. Dhamira ya kishazi kijalizo ni kutoa taarifa, kuamrisha, kuuliza maswali au kushangaa.

(44)


a. Nilijua [kuwa ungekuja.] (taarifa).

b. Hakimu aliamuru [kuwa afungwe jela.] (amri)


c. Aliniuliza [kama nilikuwa nikiondoka.] (swali)

Uwakilishi wake kwenye kielelezo tungo utakuwa katika 45 (a), (b), na c.


45 (a)




(b)




(c)




Katika michoro 45(a), (b), na (c) $\overline{S}$ (kishazi kijalizi) ni dada ya T na kwa hivyo kinapanua T hadi $\overline{T}$. Hii ni nafasi ya kijalizo.

Vitenzi huchagua vishazi vijalizo kwa misingi ya semantiki (maana). Bresnan (1979:67), akinukuliwa na Radford (1988) anadai kuwa kishazi kijalizo cha maswali hutokea pamoja na kitenzi cha maswali. Kwa mfano:

a. Nitauliza [iwapo Linda atakuja].

b. Tunashuku [endapo ataweza].

c. Walijadili [kama wangefikia uamuzi mwafaka].

Vitenzi vya utambuzi kama vile ( jua, hisi, fikiri, tambua, wazia), na vitenzi vya kutetea kama (sema, dai, tangaza) kwa ujumla huchukua vijalizo vinavyoarifu au vinavyoonyesha kama tunavyoona katika (45) hapa chini:

(46)

a. **Ninajua** [kwamba mimi ni sahihi]

b. Ni lazima **ujue** [kuwa umekosa]

c. **Ninafikiria** [kuwa umechoka]

d. **Alidai** [kwamba hakufanya kosa]

Maneno kama vile “kuwa, iwapo, kwamba, kwa kuwa” hutumiwa kutanguliza vishazi vijalizo.

### 3.3.3 KIJALIZO CHA KIHUSISHI.

Kijalizo cha kihusishi ni kijalizo ambacho ukamilishi wake hurejea kwenye kihusishi. Kihusishi ni neno ambalo huonyesha uhusiano uliopo kati ya nomino/ kiwakilishi na neno/ maneno mengine yaliyopo katika sentensi hiyo. Edmonds (1976:172), akinukuliwa na Radford (1988:363) alisema kuwa, vihusishi vina majukumu makubwa zaidi katika sintaksia kuliko ilivyochukuliwa katika sarufi ya kimapokeo. Kihusishi huonyesha uhusiano wa kiwakati, uhusiano wa mahali, uhusiano wa kulinganisha, uhusiano wa umilikaji, uhusiano wa kitu na aina/ sampuli yake.


Kwa kawaida kihusishi huja kabla ya nomino/ kiwakilishi au virai nomino. Kwa mfano.

(47) (a) Mlevi amelala *chini ya* (H) *mtaro* (N).

(b) Wageni wamefika *baada ya* (H)*wale waheshimiwa* (N).

Katika 47 (a) [chini ya] ni kihusishi na mtaro ni nomino inayojaliza kihusishi [chini ya]. Katika 47(b) [baada ya] ni kihusishi na kinajalizwa na kirai nomino [wale waheshimiwa]. Uwakilishi wa sentensi 47(b) kwenye kielelezo tungo ni:

48




Katika mchoro 48 (b), KN ni dada ya H na kwa hivyo kinapanua H hadi $\overline{H}$ na kama tulivyokwisha kusema, hili ni jukumu la kijalizo.

Nomino au kiwakilishi kinachokuja baada ya kihusishi huitwa *yambwa ya kihusishi* (Matei 2008:74) lakini sisi tunaita *kijalizo*. Huitwa hivyo kwa sababu ndiyo ambayo kihusishi katika sentensi inailenga kwa kuihusisha na nomino au kipashio cha awali. Kwa mfano katika sentensi "Vitabu vipo juu ya rafu," 'rafu' ndiyo kijalizo cha kihusishi 'juu ya'. Kihusishi 'juu ya' kinahusisha vitabu na rafu kwa kuonyesha mahali vitabu vipo.

Vihusishi huweza kuwa sahili. Hivi ni vihusishi ambavyo kwa kawaida huwa ni neno moja kama vile kwa, hadi, mpaka, tangu. Kwa mfano:

(a) Babu huishi *kwa* mama.

(b) Sijamwona Maria *tangu* juzi.

Vihusishi pia huweza kuwa changamano. Hivi huwa na maneno mawili au matatu ambayo hutumiwa pamoja kuonyesha uhusiano kati ya vipashio viwili katika sentensi. Kwa mfano:

(a) Lulu alikuwa *miongoni mwa* waliotuzwa.

(b) Tutaketi *mbele ya* wasimamizi wetu.

Vihusishi pia huweza kutumiwa kama vielezi. Kwa mfano: Nitakueleza *baadaye* (kielezi).

Vihusishi vilevile huonyesha mtenda/ kitenda/ kifaa. Kwa mfano:

(a) Kazi hiyo imefanywa *na* mfanyikazi hodari.

(b) Alipika wali *kwa* sufuria.

Cowper (1992:23), anasema kuwa tunaweza kuchukulia kuwa, kuna vihusishi elekezi na vihusishi visoelekezi kama vilivyo vitenzi elekezi na vitenzi visoelekezi.

**Vihusishi elekezi:** Ni vihusishi ambavyo lazima vichukue vijalizo. Vijalizo hivi vinaweza kuwa nomino au kirai nomino, kielezi au kirai elezi, kivumishi au kirai vumishi na kishazi kijalizi. Kwa mfano.

49 (a) Mtoto amelala chini ya *meza.* (N)

(b) Mtoto amelala chini ya *meza kubwa*. (KN)

(c)Alifundisha mbele ya *wajinga* (V)

(d) Alifundisha mbele ya *wajinga wengi* (KV)

(e) Nimewasubiri tangu *jana* (E)

(f) Nimewasubiri tangu *jana asubuhi* (KE)

(g) Nilimngoja *mpaka nikachoka* ($\bar{S}$)

Katika 49(a), kijalizo cha kihusishi *chini ya* ni nomino ‘meza’ na katika 57(b), kijalizi cha kihusishi *chini ya* ni ‘meza kubwa’. Katika 49(c) na (d), kijalizi cha kihusishi ‘mbele ya’, ni kivumishi ‘wajinga’ na kirai vumishi ‘wajinga wengi’ mtawalia. Sentensi 49(e) na ((f)

kijalizo cha kihusishi tangu ni kielezi ‘jana’ na kirai elezi ‘jana asubuhi’. Katika (49) (g), kihusishi ni *mpaka* na kijalizo chake ni kishazi kijalizi *nikachoka*

**Vihusishi visoelekezi :** Ni vihusishi visivyohitaji kijalizo kukamilika kimawasiliano. Muundo wake haudokezi uwezekano wa kuwa na kijalizo. Kwa mfano.

(50) (a) Sinia iko *chini.*

(b) Nitakuja *baadaye.*

‘Baadaye’ na ‘chini’ katika sentensi (50) (a) na (b) ni vihusishi visoelekezi kwa sababu havihitaji vijalizo ili vikamilishe maana.

**Vihusishi vyenye sifa zote mbili za uelekezi**: Kuna vihusishi vilivyo na sifa zote mbili za uelekezi. Hivi ni vihusishi ambavyo vinaweza kutumika pasi na kijalizo na wakati mwingine vikatumika pamoja na kijalizo. Kwa mfano:

51 (a) Weka hicho kiti *chini*.

(b) Weka hicho kiti *chini ya meza*.

Katika 51 (a), *chini* ni kihusishi kisoelekezi lakini katika 51(b) limetumiwa kama kihusishi elekezi kinachohitaji kijalizo ili maana ikamilike.

### 3.3.3.1 UTEUZI WA VIJALIZO KATIKA VIHUSISHI.

Vihusishi kama vitenzi vina sifa ya uteuzi ijapokuwa sifa yake ni telezi mno na haiwezi kuwekewa sifa moja jumlishi kama vilivyo vitenzi. Itabidi tuchunguze vihusishi vichache tu kinyume na vitenzi. Vihusishi hujalizwa na:

(a) Nomino au kirai nomino.

(b) Kielezi au kirai elezi.

(c) Kihusishi au kirai husishi.

(d) Kishazi kijalizo.

### 3.3.3.2 KN, KE ($\bar{s}$) NA Ø KAMA VIJALIZO VYA KIHUSISHI.

Zingatia sentensi 52(a),(b) na (c).

(52)(a) Sijamwona [tangu ile sherehe].

(b) Sijamwona [tangu kuanza kwa ile sherehe].

(c) Sijamwona [tangu].


Kihusishi 'tangu' ni kihusishi ambacho kinachukua kijalizo cha KN[ile sherehe] katika 52(a) na kinachukua kishazi kijalizi ($\bar{s}$) [ kuanza kwa ile sherehe] katika 52(b) na kijalizo Ø katika 52(c) Iwapo hivi ndivyo ilivyo, basi uteuzi wake utaonekana hivi:

Tangu: sifa za kategoria: [-T,-N];

Sifa za uteuzi: [____ [KN],[$\bar{s}$],[Ø]]


Kihusishi *tangu* kinachukua nafasi iliyoonyeshwa kwa kistari kirefu. Kwa hivyo kihusishi *tangu* kinachukua aina tatu za vijalizo: KN,$\bar{s}$ na Ø kama inavyodhihirika katika (52) hapo juu. Uwakilishi wa 52(a), (b) na (c) katika kielelezo tungo 53(a), (b), na(c).

53( a)





Mchoro 53 (a), unaonyesha kuwa KN (ile sherehe) ni dada ya H (tangu) na kwa hivyo KN ni kijalizo cha H na kinapanua H hadi $\overline{H}$ na $\overline{H}$ kinajipanua hadi KH.

(b)



(c)




Katika mchoro 53(a) na 53(b) KN ni dada ya H na kinapanua H hadi $\overline{H}$ lakini katika 53(c) H kinajipanua hadi $\overline{H}$ kwa sababu hakina kijalizo.

Vihusishi vingine hata hivyo, vinachukua vijalizo vichache. Kwa mfano, kihusishi ‘mpaka’ kinaweza kuchukua kijalizo cha KN au cha KE au kishazi kijalizi ($\bar{s}$) lakini hakiwezi kuchukua kijalizi kapa (Ø). Hakiwezi kuchukua kijalizi Ø kwa sababu ni kihusishi elekezi. Tazama sentensi (54):


54) (a) Alingoja [mpaka Jumamosi] KN/KE.

(b) Alingoja mpaka [akaondoka] $\bar{s}$

(c)*Alingoja [mpaka]


Kihusishi *mpaka* katika sentensi 54 (a) kinajalizwa na KN/KE na katika 54 (b) kinajalizwa kwa kishazi kijalizi ($\bar{s}$) lakini hakiwezi kuchukua kijalizo kapa kwa sababu kinapochukua kijalizo kapa, usarufi wa sentensi unapotea. Uwakilishi wa 54(a) na (b) kwenye kielelezo tungo utakuwa 55 (a) na (b) hapa chini:

55 (a)




Kwenye mchoro 55 (a), KE (Jumamosi) ni dada ya H (mpaka) na kwa hivyo kinapanua H hadi $\overline{H}$ . Hili ni jukumu la kijalizo (KE ni kijalizo cha H)

55 (b)




Katika kielelezo tungo 55 (b), kishazi kijalizi ($\bar{s}$) ni dada ya H na kwa hivyo ni kijalizo cha H. kinapanua H hadi $\overline{H}$.

Kihusishi ‘chini’ kinachukua kijalizo KN lakini hakichukui kishazi kijalizi ($\bar{s}$). Hata hivyo kinaweza kuchukua kijalizo kapa (Ø). Kwa mfano:

56 (a) Mtoto alilala [chini] (Ø)

(b) Mtoto alilala [chini ya mti] KN

Kihusishi *chini* katika 56 (a) kimechukua kijalizo Ø ilhali katika 56 (b) kimechukua kijalizo KN.


### 3.3.3.3 KIHUSISHI KAMA KIJALIZO CHA KIHUSISHI KINGINE.

Ijapokuwa tumeangazia tu vihusishi vinavyochukua vijalizo vya [KN], [KE], [Ø] na $\bar{s}$ kuna kikundi kingine cha vihusishi kinachochukua vijalizo ambavyo ni vihusishi (Radford1988:364). Kihusishi kinajaliza kihusishi kingine. Kwa mfano:

57(a) Alikaa nyumbani *kwa sababu* [ya mgomo]

Katika sentensi 57(a) kihusishi ‘kwa sababu’ kinajalizwa kwa kihusishi [ya mgomo]. Uwakilishi wake kwenye kielelezo tungo utakuwa kama ifuatavyo:

58




Katika mchoro (58), KH ni dada ya H na kinapanua H hadi kiwango cha $\overline{H}$ kama kifanyavyo kijalizo.

### 3.3.4 VIJALIZO VYA VIVUMISHI.

Kijalizo cha kivumishi ni kijalizo ambacho ukamilishi wake hurejea kwenye kivumishi.Kivumishi huwa na sifa za uelekezi kama zilivyo vitenzi. Kuna vivumishi ambavyo lazima vichukue vijalizo ili maana yake iwe kamili. Kivumishi ni neno au maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu nomino/ kiwakilishi (hufafanua nomino). Kuna aina nyingi za vivumishi kama vile; Kivumishi cha sifa, kivumishi kiashiria, kivumishi kimilikishi, kivumishi cha pekee, kivumishi kirejeshi, kivumishi cha ‘a’ unganifu, kivumishi jina. Vivumishi hivi ni vingi lakini si vyote vinavyohitaji kijalizo.


Kivumishi ‘a’ unganifu huhitaji kijalizo ili kiweze kukamilika (Mbesa 2008:76). Nafasi hii ya kijalizo huchukuliwa mara nyingi na KN na wakati mwingine kishazi kijalizi ($\bar{s}$). Kwa mfano:

59(a) Wanafunzi wa *shule jirani* wametoroka

(b) Arusi ya *aliyekuwa mkuu wa shule imefanywa.*


Katika 59(a) na (b) maneno ‘wa’ na ‘ya’ ni vivumishi vya ‘a’ unganifu na vinajalizwa na KN na $\bar{s}$ (kishazi kijalizi) mtawalia. Uwasilishi wa 59(b) kwenye kielelezo cha matawi.

60 (a)



60 (a) ni mchoro unaoonyesha kuwa KN (shule jirani) ni kijalizo cha kivumishi (wa). KN kinapanua V hadi $\bar{V}$ na ndilo jukumu la kijalizo.

(b)




Kwenye kielelezo tungo 60 (b), kishazi kijalizi ($\bar{s}$) ni dada ya V(kivumishi) na kwa hivyo kinapanua V hadi $\bar{V}$. Kishazi kijalizi ($\bar{s}$) ni kijalizo cha V.


Kivumishi cha pekee – enye pia ni kivumishi ambacho huhitaji kijalizo. Mara nyingi kijalizo cha kivumishi hiki huwa ni KN. Kwa mfano:

61(a) Mtu mwenye *nyumba nzuri* amesafiri ng'ambo.

(b)Watoto wenye *kucheza huwa na afya.*

Uwakilishi wa 61(a) katika kielelzo tungo:

62




KN katika (62) ni kijalizo cha kivumishi –enye. KN ni dada ya V na kwa hivyo kinapanua V hadi $\bar{V}$.

Haiwezekani kutumia kivumishi cha pekee –enye bila kutumia pamoja na kijalizo chake. Kwa mfano.

(62) *Mtu mwenye amesafiri ng’ambo.

Sentensi (62) imevurugika kisarufi na usanifu wake utajitokeza tu iwapo kijalizo cha kivumishi –enye kitatumika. Kivumishi cha pekee –enye ni kivumishi kinacholeta dhana ya umilikaji na kinapotumika, lazima kifuatwe na nomino inayomilikiwa. Nomino inayotumika kuonyesha umilikaji katika kivumishi –enye ndiyo tunayoita kijalizo.

### 3.3.5 HITIMISHO.

Katika sura hii, tumefafanua miundo tofauti ya kijalizo. Tukasema kuwa kijalizo kinaweza kutokea kama nomino au kirai nomino, kivumishi au kirai vumishi, kitenzi au kirai tenzi, kielezi au kirai elezi, kihusishi au kirai husishi na kishazi kijalizi. Tumefafanua miundo hii kwa kutumia vielelezo tungo.

Tumefafanua pia aina tofauti za vijalizo kama vile kijalizo cha nomino, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha kihusishi na kijalizo cha kivumishi kwa msingi wa nadharia ya $\overline{X}$. Hujalizwa kwa nomino au kirai nomino, kivumishi au kirai vumishi, kihusishi au kirai husishi, kitenzi au kirai tenzi kwa kutegemea sifa za uteuzi. Tukasema kuwa uteuzi ni uwezo wa kategoria za maneno wa kuchagua aina za vijalizo vya kuchukua. Tumechanganua aina za vijalizo katika kielelezo tungo kwa msingi wa nadharia ya x-baa.

## 4.0 MATOKEO NA HITIMISHO.

### 4.1 UTANGULIZI.

Katika sura ya tatu tulifafanua miundo na aina tofauti za kijalizo. Miundo ya kijalizo cha Kiswahili sanifu na pamoja na: nomino au kirai nomino, kitenzi au kirai tenzi, kivumishi au kirai vumishi, kihusishi au kirai husishi, kielezi au kirai elezi na kishazi kijalizi. Aina za vijalizo ni pamoja na: kijalizo cha nomino, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha kihusishi na kijalizo cha kivumishi. Katika sura ya nne tutatamatisha kazi yetu kwa kutoa matokeo ya utafiti wetu, kutoa mapendekezo na kuhitimisha kazi yetu.

### 4.2 MATOKEO YA UTAFITI.

Katika nadharia tete, tulitarajia kuwa tafsili ya kijalizo cha Kiswahili ni pana zaidi kuliko ilivyoelezwa na wanaisimu wa Kiswahili. Tuligundua kuwa dhana ya kijalizo hueleweka kwa njia nyingi kutegemea mwelekeo wa nadharia inayotumiwa. Kijalizo katika sarufi mapokeo kilichukuliwa kuwa neno au fungu la maneno linalotokea baada ya kitenzi kishirikishi.

Katika utafiti wetu, tumetumia nadharia ya x-baa kufafanua kijalizo. Kijalizo katika nadharia ya x-baa ni neno au fungu la maneno linalofungamanishwa moja kwa moja na kichwa cha kirai husika (dada ya kichwa cha kirai). Kijalizo hupanua kichwa cha kirai hadi kiwango kingine. Kwa mfano: Funga *huo mlango*. Maneno kwenye mlazo ni kijalizo cha kitenzi 'funga'.

Tumethibitisha pia kuwa kijalizo si kipashio cha kirai tenzi pekee bali ni kipashio cha kirai nomino, kirai vumishi, na kirai husishi.

Tulibashiri pia kuwa kuna kanuni zinazotawala uunganishwaji wa vipashio vya kijalizo na viungo vingine kwenye tungo. Tulitambua kuwa kijalizo hufungamanishwa na kichwa cha

kirai na kinapotenganishwa na kichwa cha kirai, basi si kijalizo tena bali ni chagizo. Kwa mfano:

(a) Kiti **cha babu** kimevunjika.

(b) Kiti kirefu, kizee **cha babu** kimevunjika.

Katika (a) *cha babu* ni kijalizo cha *kiti* kwa sababu kimefungamanishwa na kichwa cha kirai na kinapanua *kiti*kiwango kingine ambacho ni *kiti cha babu.*Katika sentensi (b) *cha babu* ni chagizo na wala si kijalizo kwa sababu kimesongeshwa mbali na kichwa cha kirai husika.

Haipothesia yetu nyingine ilikuwa ni kuwa aina za vijalizo ni zaidi ya mbili. Utafiti wetu umedhihirisha kuwa ni kweli. Tumechanganua aina zaidi ya mbili ya vijalizo vya Kiswahili sanifu. Aina hizi ni pamoja na: kijalizo cha nomino, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha kihusishi, na kijalizo cha kivumishi.

Tulidhamiria kuwa nadharia ya x-baa ingefaa katika kuchanganua kijalizo cha Kiswahili sanifu. Matokeo ni kuwa kwa hakika nadharia ya x-baa ilifaa sana katika uchanganuzi wa kijalizo. Nadharia ya x-baa inatambua nafasi ya kijalizo katika kirai na nafasi hiyo ni kuwa kimefungamanishwa na kichwa cha kirai. Jukumu la kijalizo katika nadharia ya x-baa ni kupanua kichwa cha kirai hadi kiwango kingine (hupanua X hadi $\bar{X}$ ).

## 4.3 MAPENDEKEZO.

Katika utafiti wetu, tulipata mapengo kadhaa yaliyostahili kujazwa na hatungeweza kujaza. Tuligundua kuwa chagizo kinastahili kufanyiwa utafiti wa kina kwa kutumia nadharia ya x-baa. Tunapendekeza utafiti wa chagizo kwa kutumia nadharia ya x-baa.

Mada yetu pia ambayo ni *sintaksia ya kijalizo cha Kiswahili sanifu* inaweza pia kufanyiwa utafiti kwa kutumia nadharia nyingine kama vile Uminimalisti.

## 4.4 HITIMISHO.

Utafiti wetu umehusu sintaksia ya kijalizo cha Kiswahili sanifu. Tumeeleza maana ya kijalizo kwa misingi ya nadharia ya x-baa. Tumechanganua miundo tofauti ya kijalizo pamoja na aina za kijalizo tukizingati nadharia ya x-baa. Tumetumia kielelezo tungo kufafanua kijalizo. tumetambua kuwa maana na jukumu la kijalizo hutegemea nadharia inayotumika kukifafanua. Idadi ya aina za vijalizo pia hutegemea mtazamo wa nadharia anayotumia mtu. Mtu akitumia nadharia ya sarufi mapokeo, kuna aina mbili tu za vijalizo : kijalizo cha kiima na kijalizo cha yambwa na anapotumia nadharia ya x-baa, aina za vijalizo ni: kijalizo cha nomino, kijalizo cha kitenzi, kijalizo cha kihusishi, kijalizo  cha kivumishi.

**MAREJELEO.**

Arege, T na Matei, A. (2006)*Kunga za Kiswahili.* Nairobi: Focus.

Chomsky, N. (1965) *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge : MIT Press.

Crystal, D. (1991) *The Cambridge Encyclopaedia of Languages.* New York: O.U.P.

Cowper, E. (1992) *A Concise Introduction to Syntactic Theory: The Government-Binding Approach*: Chicago, The University of Chicago Press.

Culicover, P. (1976) *Syntax.* New York, Academic Press.

Haegeman, L. (1991) *Introduction to Government and Binding Theory:*U K, Blackwell Publishers.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix.

Habwe, J. na Matei, A. (2006) *Darubini ya Kiswahili, Marudio Kamili* ya KCSE, Nairobi,Phoenix.

Ipara, I na Wengine. (2010) *Upeo wa sarufi.* Nairobi : Oxford University Press.

Jerono, P. (2003) “Kishazi huru Arifu cha Kiswahili: Mtazamo wa X-baa” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Kirubi, J na wengine (2007) *Gateway KCSE (Kiswahili)* Nairobi: Longhorn.

Longhorn (2011) *Kamusi ya Karne ya 21.*Nairobi: Longhorn.

Massamba, D.P.B (2004) *Kamusi ya Falsafa na Isimu*. Dar-es-salaam: TUKI

Matei, A. (2008) *Sarufi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Mukhwana, A. na Obuchi, S.(2010) *Muundo wa Kiswahili Ngazi na Vipengele.* Nairobi: Frame Publishers.

Mumbo, K. na Ngamia, O. (2005) *Johari ya Kiswahili* . Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mbesa, N. (2008) Mofosintaksi ya Kishazi Nomino cha Kiswahili sanifu: Mtazamo wa X-baa. Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mgullu, R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn.

Nyaga, L. (2011) Mofosintaksi ya kishazi kielezi cha Kiswahili sanifu: Mtazamo wa X-baa. Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Olali, T. (1998) Kirai nomino cha Kiswahili: Mtazamo wa X-baa" Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi . (Haijachapishwa).

Poole, G. (2002) *Syntactic Theory:*New York, Palgrave Houndmills, Basingstoke.

Radford, A. (2004) *English Syntax: An introduction.* Cambridge Cambridge University Press.

_____________(1988) *Transformational Grammar*:Great Britain, Cambridge University Press.

Ramsay, F. na wengine (1995)*The Glossary of the Little Brown Handbook, 6th ed:* New, YorkHarper Collins

Wamitila K.W (2004) *Chemchemi za Kiswahili.* Nairobi: Longhorn.